# MCHANGO WA VIJANA KATIKA KULETA MABADILIKO KATIKA *KUFA KUZIKANA* NA *KIDAGAA KIMEMWOZEA*

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

**FLORENCE MUTHIO MUNYASYA**

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

**TASNIFU HII IMETOLEWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

A1701236A
University of Nairobi Library Thesis
2016

**2017**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi ____________________ Tarehe 15/11/2017

**Florence Muthio Munyasya**

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi ____________________ Tarehe 15-11-17

**Dkt. Evans M. Mbuthia**

(Msimamizi)

Sahihi ____________________ Tarehe 15/11/2017

**Bw. Samson Ongarora**

(Msimamizi)

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu; marehemu babangu mpendwa Benjamin Munyasya aliyeniwekea msingi imara katika masomo yangu na mama yangu Damaris Kasyoka Benjamin kwa kunilea vizuri na kunipa msingi mzuri wa maisha.

# SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya na uwezo. Shukrani pia ni kwa wasimamizi wangu Dkt. Evans M. Mbuthia na Bw. Samson Ongarora kwa kunielekeza vema ili kuandika kazi hii. Nawashukuru wahadhiri wote walionifundisha. Hawa ni: Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Habwe, prof. Mbatia, Prof. Rayya Timmamy, Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Omboga Zaja, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Jerono Prisca na Dkt. Amiri Swaleh.

Nawashukuru wasomi wenzangu tuliosoma pamoja kwa kunifaa katika mijadala na ushauri hasa Tekla Kiptum kwa kunipa bega la kuegemea wakati maisha yalipokuwa magumu. Mungu awafanikishe maishani mwenu. Pia natoa shukrani za dhati kwa mume wangu Shadrack Musyimi, watoto wangu Dennis Munyasya na Mark Muvea kwa kunivumilia na kunihimiza wakati nilikuwa nikisoma.

# IKISIRI

Katika utafiti huu, tumeonyesha mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*. Pia, tumeangazia changamoto ambazo vijana hukumbana nazo katika juhudi zao za kuleta mabadiliko. Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii ambao unajihusisha na utetezi wa wanyonge na ukombozi wao. Tumetambua kwamba vijana ni mawakala wa mabadiliko na wanaweza kuleta mchango ambao unaweza kuwafaidi wanajamii wote. Hii ni kwa sababu vijana ni wenye nguvu za mwili na maarifa ambayo wanaweza kutumia ili kuifunza jamii. Pamoja na haya, tumeonyesha kwamba vijana wanakabiliana na changamoto nyingi ambazo ni lazima zichukuliwe hatua ili kizazi hiki ambacho ni muhimu sana kipate kuokolewa. Tulitumia mbinu za utafiti za maktabani na mtandaoni. Maktabani, tulisoma riwaya mbili teule na makala tofauti kama vile tasnifu na vitabu vyenye maelezo kuhusu nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Tulitembelea mtandao na kuangalia masuala yanayohusiana na vijana na pia tulisoma maelezo kuhusu nadharia ya uyakinifu wa kijamii.

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii

TABARUKU ........ iii

SHUKRANI ........ iv

IKISIRI ........ vi

YALIYOMO ........ v

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Tatizo la utafiti ........ 3

1.3 Maswali ya utafiti ........ 4

1.4 Malengo ya utafiti ........ 4

1.5 Sababu za kuchagua mada ........ 4

1.6 Upeo na mipaka ........ 5

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 5

1.8 Msingi wa kinadharia ........ 10

1.8.1 Usuli wa nadharia ya uyakinifu wa kijamii ........ 10

1.8.2 Mihimili ya uyakinifu wa kijamii ........ 11

1.9 Mbinu za utafiti ........ 13

1.10 Hitimisho ........ 14

**SURA YA PILI**

SUALA LA VIJANA NA MABADILIKO KATIKA *KUFA KUZIKANA* NA *KIDAGAA KIMEMWOZEA* ........ 15

2.1 Utangulizi ........ 15

2.2 Utawala mbaya na ufisadi ........ 16

2.3 Tamaduni potovu zilizopitwa na wakati ........ 25

2.4 Ukabila ........ 29

2.5 Mtazamo kuhusu walemavu ........ 33

2.6 Mitazamo ya watu kuhusu maisha ........ 34

2.7 Wizi wa miswada ........ 37

2.8 Unyanyasaji wa wanyonge ........ 39

2.9 Umuhimu wa haki za watoto ........ 40

2.10 Kisasi na msamaha ........ 40

2.11 Hitimisho ........ 41

SURA YA TATU

CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA VIJANA KATIKA HARAKATI ZA KULETA MABADILIKO KATIKA *KUFA KUZIKANA* NA *KIDAGAA KIMEMWOZEA ZA* KEN WALIBORA ........ 43

3.1 Utangulizi ........ 43

3.2 Ulemavu ........ 43

3.3 Uyatima ........ 45

3.4 Kukatizwa kwa masomo ya vijana ........ 47

3.5 Umaskini ........ 51

3.6 Mihadarati na pombe ........ 54

3.7 Mapenzi ya kiholela ........ 55

3.8 Mila na imani zilizopitwa na wakati ........ 58

3.9 Ukosefu wa sera madhubuti za kuwatuza wanamichezo ........ 61

3.10 Ukosefu wa umoja na ari ya kuleta mabadiliko ........ 62

3.11 Chuki na fitina ........ 63

3.12 Hitimisho ........ 65

SURA YA NNE

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

4.1 Utangulizi ... 66

4.2 Muhtasari wa matokeo ... 66

4.3 Hitimisho ... 67

4.4 Mapendekezo ... 68

**MAREJELEO** ... 70

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti wetu ulihusu ubainishaji wa mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*. Pia, tulinuia kuangazia changamoto ambazo vijana hukumbana nazo katika harakati zao za kuleta mabadiliko katika riwaya hizi teule. Ili kuelewa vizuri suala la vijana katika riwaya hizi mbili, ni vizuri kwanza kufahamu dhana ya neno kijana na mambo yanayohusiana na vijana. Neno kijana linaweza kutolewa fasili tofauti tofauti kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile kigezo cha ki- umri, kijamii na hata kiuchumi.

Kwa kuzingatia kigezo cha ki-umri, nchini Kenya, sera ya kitaifa kuhusu vijana inawaeleza vijana kama watu wa jinsia zote mbili ambao umri wao ni kati ya miaka kumi na mitano na thelathini. Haya yanatokana na tarakimu za Wizara ya Vijana na Michezo iliyobuniwa mwaka wa 2008. Katiba ya nchi ya Kenya (2010) inamwelezea kijana kama mwananchi wa umri kati ya miaka 18 hadi 35.

Makala ya Chepkwony (2005) yanayoitwa "Vijana: Changamoto kwa kanisa katika Afrika ya leo", yanaeleza ujana kama kipindi kilichojaa uhai kati ya utoto na utu uzima. Kundi hili la binadamu ni muhimu kwa sababu ndio wanategemewa kuendeleza kizazi cha kesho. Kwa hivyo, watu wazima wanapaswa kuwafunza vijana amali na tamaduni za jamii. Kwa sababu hii, vijana wanashinikizwa kukubali na kufuata vigezo na mahitaji ya jamii kwa sababu sehemu kubwa kati yao haikubaliani na matakwa haya.

Kutokana na fasili hizi mbalimbali za neno kijana, tunapata kuwa kuna mkanganyo katika kuamua kipindi cha ujana huanzia wapi na kuishia wapi. Hata hivyo, katika kazi hii, tutaangalia vijana kulingana na jinsi mwandishi amewasawiri na pia kwa kuzingatia baadhi ya majukumu aliyowapatia vijana. Zaidi ya hayo, mwandishi ameonyesha umri halisi wa baadhi ya wahusika ambao ni vijana. Kwa mfano, Amani alikuwa na miaka 24, Tim alikuwa na miaka 20 na Pam alikuwa na miaka 21. Katika kazi hii, tulimchukulia kijana kama binadamu wa kiume au kike aliye na umri kati ya miaka 15 hadi 35. Vijana waliorejelewa katika riwaya teule wana umri huu wa kati ya miaka 15 hadi 35.

Utafiti wetu kwa upande ule mwingine ulishughulikia suala la mabadiliko, ambalo pia huwa ni tata. Utata huu unatokana na sababu kuwa, mabadiliko yanaweza kuwa chanya au hasi. Utata kuhusu mabadiliko hutokea kwa sababu kuna watu ambao hupuuza mabadiliko hata yale ambayo ni chanya kama hayafuati maadili ya jamii. Mabadiliko katika jamii ni lazima yatokee na jinsi jamii inavyobadilika ndivyo vijana wanavyobadilisha majukumu yao. Mfumo wa zamani wa maisha umebadilika na hivyo kuyabadilisha majukumu ya vijana. Maisha ya kiasili ya Mwafrika yalihusu jamii nzima na watoto walikuwa mali ya jamii nzima.

Mabadiliko katika jamii yamevuruga mfumo huu wa maisha na kuwaacha vijana na changamoto nyingi. Elimu ya kimagharibi imeathiri mtagusano uliokuwepo katika jamii na kusababisha mabadiliko makubwa katika thamani na maadili ya jamii. Mabadiliko tuliyoyashughulikia katika utafiti wetu ni yale yanayotokana na kuvunjwa kwa maadili ya kijamii yanayopelekea kuwa na mifumo dhalimu, vita vya kikabila, matumizi mabaya ya mali ya umma, mtazamo mbaya kuhusu walemavu na maovu mengineyo.

Utafiti huu ulidhamiria kuonyesha kuwa wahusika vijana wana uwezo wa kuwa mawakala wa mabadiliko na wakafanikiwa. Katika kazi tulizozichambua, vijana wamesawiriwa kama wanajamii waliojitolea ili kuleta mabadiliko chanya yatakayowafaidi wanajamii wote wanaodhulumiwa kwa njia mbalimbali. Watu hutekeleza mapinduzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa sababu ya kutoridhika na jinsi ambavyo wanatawaliwa au kwa kuichukia mifumo fulani ya watu inayowakandamiza na kudumisha maslahi ya watu wachache wenye vyeo na mamlaka.

Vijana huwa wanakabiliwa na changamoto nyingi sana katika kipindi hiki cha ujana. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu vijana (2005), vijana huwa wanaathirika sana na matatizo haya kuliko wanajamii wale wengine. Ripoti hii ya Shirika la Umoja wa Mataifa ina mtazamo chanya kuhusu vijana kwa sababu inaonyesha kuwa vijana ni muhimu sana kwa kutatua matatizo yanayowakabili. Wanaonekana kuwa na nafasi nzuri katika kushughulikia hali zao kuliko wanajamii wengine. Ripoti hii inaonyesha vijana kuwa katika msukumo wa mabadiliko na wana sauti yenye nguvu kuhusu haki zao na jinsi ya kukabili na kutatua changamoto zinazowakumba. Baadhi ya vijana wana mtazamo mpya kuhusu maisha na wamekuwa msitari wa mbele katika kusuluhisha changamoto za kimaendeleo. Matatizo haya yanayowakabili hususan vijana ni kama elimu duni, kutoshirikishwa katika kufanya

maamuzi, dawa za kulevya, ugonjwa wa ukimwi, teknolojia, ukosefu wa ajira, mmomonyoko wa maadili, umaskini, ubaguzi wa kijinsia na mengineyo mengi. Kwa hivyo, kupitia kampeni za uhamasisho, vijana wanakuwa ni watatuzi wa matatizo yao bali si sehemu ya matatizo haya.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Vijana ni kundi la binadamu ambalo ni muhimu sana kwa sababu wanaweza kuchangia vizuri upande wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika karne ya ishirini, baadhi ya waandishi wa kazi za fasihi waliangazia vijana kwa mtazamo hasi na kuwaona kama watu wasiojiweza. Waliwasawiri kama watu waasi wasioweza kuleta mchango wowote wa kimaendeleo. Katika karne ya ishirini na moja, kuna mwamko kuhusu umuhimu wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya. Mashirika mbalimbali yameanza kutetea maslahi ya vijana. Kwa mfano, tarehe kumi na mbili Agosti ni siku ya vijana duniani inayonuia kuangazia mchango na changamoto zinazowakumba.

Mwandishi wa *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea,* amebuni wahusika vijana wanaotoa mchango mkubwa katika riwaya zake. Utafiti huu unahusu ubainishaji wa mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko, kwa kuchunguza riwaya mbili za Ken Walibora ambazo ni *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*.

Katika karne ya ishirini na moja, kuna changamoto nyingi ambazo vijana wanakabiliana nazo. Changamoto hizi zinaweza kuwaathiri vijana vibaya sana kama hazitashughulikiwa. Fasihi kama kioo cha jamii ni njia nzuri ya kuangaza changamoto hizi ili wanajamii waweze kuzitambua na kukabiliana nazo. Baadhi ya masuala haya yamejitokeza katika kazi tulizozitafiti.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Vijana wametoa mchango gani wa kuleta mabadiliko katika *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*?

ii) Ni changamoto zipi zinazowakabili vijana katika juhudi zao za kuleta mabadiliko?

## 1.4 Malengo ya utafiti

Malengo ya utafiti huu ni:

i) Kuchunguza mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*.

ii) Kuangazia changamoto ambazo huwakabili vijana katika juhudi za kutaka kuleta mabadiliko, katika *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*.

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Tulichagua mada hii kwa sababu kadhaa. Kwanza tulitaka kuonyesha umuhimu wa vijana. Vijana huwakilisha kizazi chenye nguvu za mwili na maarifa mapya. Kwa hivyo, wakipewa nafasi wanaweza kuleta mabadiliko yatakayowafaidi wanajamii. Maelezo ya Wafula (1999) yanadhihirisha umuhimu huu wa vijana. Vijana wakiwepo, jamii hupata uhai wake, kwani huendeleza vizazi na vizazi.

Sababu nyingine ni kuwa, baadhi ya waandishi wamekuwa hawathamini mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko ya kimaendeleo. Hili limetokana na dhana-gande kuwa vijana ni watu ambao hawawezi kujisimamia ki mawazo na hata kimatendo. Kwa hivyo, waandishi wanapaswa kubadili huu mtazamo na kuanza kuwathamini vijana kwa kuwapatia nafasi ya kuchangia katika ujenzi wa taifa.

Fauka ya hayo, kumekuwa na mwamko ambao unawahamasisha vijana kujipigania katika masuala ya jamii kama vile tamaduni zilizopitwa na wakati na ambazo zinazuia maendeleo. Hizi tamaduni ni pamoja na ndoa za mapema na za lazima, tohara ya wanawake na kadhalika. Vijana pia wameanza kujipigania kisiasa kwa kupambana na watawala wabaya na kwenda kinyume na uongozi dhalimu. Mwamko huu unapinga kasumba kuwa vijana ni

viongozi wa kesho. Kwa sababu hii, ni vizuri kuchunguza jinsi waandishi wa kazi za fasihi wamelichukulia suala hili.

Aidha, sababu nyingine ni kuwa, vijana huwakilisha uhai wa taifa. Hii inamaanisha kuwa vijana hutegemewa sana katika taifa kwa hivyo nchi ambayo haina vijana imekosa matumaini. Ukweli huu unadhihirishwa na idadi kubwa ya wazee ikilinganishwa na vijana katika baadhi ya mataifa ya ulaya, jambo ambalo limewapelekea kutoa nafasi za ajira kutoka katika mataifa yanayoendelea. Pia, tumeonyesha hali za kijamii ambazo zinagandamiza vijana na kuwazuia wasiweze kutoa michango yao ya kuijenga jamii. Fasihi ya awali inafaa kuchunguzwa upya kwa kuwa mabadiliko hutokea katika maisha ya binadamu. Mabadiliko ya kijamii yakitokea, nao waandishi hulazimika kuandika kazi zao kwa kuzingatia mambo ya wakati na mazingira yanayowazunguka. Jambo hili limetupatia ilhamu ya kufanya utafiti kuhusu mchango wa vijana katika *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea,* ili kumulika mwonoulimwengu wa waandishi kuhusu vijana hasa katika karne hii ya ishirini na moja, ambapo riwaya hizi mbili ziliandikwa.

## 1.6 Upeo na mipaka

Katika utafiti wetu, tujikita katika riwaya mbili za Ken Walibora, ambazo ni *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea.* Katika riwaya hizi, tulichunguza jinsi vijana wamechangia kuleta mabadiliko na changamoto ambazo vijana hawa wamekumbana nazo katika harakati zao za kuleta mabadiliko. Ilipobidi tulirejelea vitabu vingine vilivyoandikwa na waandishi wengine ili kutoa mifano inayohusiana na kazi yetu.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Suala la mabadiliko katika jamii za Kiafrika, lilishughulikiwa na Mazrui (1984), kwa kutumia nadharia ya ki-marx alipoihakiki riwaya ya *Dunia Mti Mkavu (1980).* Aliichanganua riwaya hiyo kwa misingi ya kisiasa na kijamii kuhusu mabadiliko na upembuzi wa jamii za Kiafrika chini ya utawala wa kikoloni. Uhakiki huu ulitufaidi kwa sababu ulishughulikia mabadiliko katika jamii za Kiafrika. Kwa hivyo, ulituwezesha kuelewa umuhimu wa

kuwepo kwa mabadiliko. Katika utafiti wetu, tulijikita katika mabadiliko yanayosababishwa na vijana.

Wa Njogu (1987), alidhamiria kuonyesha jinsi matukio ya kihistoria huathiri fasihi. Pia, alishughulikia hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii, ambazo zilizua mapinduzi ya visiwani Zanzibar. Kazi hii ilitufaa kwa sababu ilitusaidia kuonyesha jinsi vijana walileta mapinduzi katika jamii. Mapinduzi haya yalisababishwa na hali mbaya za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika kazi ambazo tumeziteua, kuna hali mbaya za kisiasa, kiuchumi na kijamii, ambazo ndizo zinazowafanya vijana kujitoa mhanga ili kupambana na hali hizi na kuleta mabadiliko yatakayowafaidi wanajamii wote.

Mitazamo ya vijana katika kujikomboa wao wenyewe ilionyeshwa na Lugano (1987), kwa kuchunguza jinsi Kezilahabi aliwasawiri wahusika wake kama vile Rosa Mistika katika *Rosa Mistika* (1971) na Kazimoto katika *Kichwa Maji* (1974). Alionyesha jinsi waling'ang'ana kuleta mabadiliko katika jamii husika. Uhakiki huu ulitusaidia kwa kuonyesha jinsi wahusika vijana wamesawiriwa katika jamii. Pamoja na haya, sisi tulishughulikia changamoto ambazo vijana wanakumbana nazo wanapojaribu kujikomboa.

Wafula (1999), alizihakiki tamthilia tatu zenye wahusika ambao ni vijana. Tamthilia hizi ni pamoja na *Wakati Ukuta* (1972), *Hatia* (1972) na *Uasi* (1980). Alitoa kauli jumuishi kuhusu vijana ambayo ni muhimu sana. Alisema kuwa vijana huweza kubadilika kwa urahisi kwa vile imani zao za kimsingi zinaendelea kujengeka. Hata hivyo, uhakiki wake haukubaini kiwango cha mabadiliko au ufanisi wa vijana katika kuinasua jamii kutokana na matatizo yenyewe. Kazi hii ni muhimu sana katika utafiti wetu kwa sababu ilishughulikia wahusika vijana ambao sisi pia tulishughulikia. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na yetu kwa sababu utafiti wetu ulionyesha ufanisi wa vijana katika kuleta mabadiliko.

Nkonge (2006), alichunguza masuala mbalimbali kuhusu vijana katika riwaya ya *Kichwa Maji* (1974) na *Nguvu ya Sala* (1999). Masuala hayo ni pamoja na mapenzi na ndoa, maisha na kifo, ulezi, uozo wa jamii na dini. Nkonge aliongozwa na nadharia ya kisosholojia kuonyesha athari za udhanaishi. Kazi hii ilitufaa katika utafiti wetu kwa sababu ilituelekeza kujua baadhi ya masuala ambayo yanaweza kuwazuia vijana wasiweze kutoa mchango wao katika ujenzi wa jamii kama vile ulezi mbaya na uozo wa jamii. Katika kazi yetu, tulionyesha

jinsi vijana wamekuwa mawakala wa mabadiliko kwa kupambana na uozo unaojitokeza katika jamii zao.

Utafiti wa Mutua (2007) ulishughulikia mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Tamthilia hizi ni pamoja na *Natala* (1997), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000), na *Migogoro* (2006). Kazi hii ni muhimu sana katika utafiti wetu kwa sababu inaonyesha jinsi vijana wamehusika katika ukombozi wa mwanamke. Hata hivyo, zaidi ya yale ambayo Mutua ameshughulikia, sisi tulishughulikia mabadiliko yaliyoletwa na vijana katika nyanja tofauti kama vile siasa, uchumi na utamaduni.

Kaui (2008), alisawiri wahusika vijana kwa kuonyesha vile nafasi yao katika jamii inaonekana kubadilika ki-mpito wakati. Alichunguza usawiri wa vijana katika tamthilia nne za Kiswahili ambazo ni *Wakati Ukuta* (1971), *Uasi* (1980), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) na *Pango* (2003). Alibaini kuwa taswira hizi ni kiwakilishi cha nia wanazotumia vijana kujipatia mamlaka na kuyatumia ili kuleta mabadiliko katika jamii. Katika kazi yake, Kaui alionyesha kuwa majukumu ya vijana katika jamii hubadilika jinsi wakati unavyopita. Kwa hivyo, waandishi wanapaswa kutilia maanani mabadiliko haya wanapoziandika kazi zao za kisanaa. Utafiti huu ulitusaidia sana katika kuyaangazia masuala yanayowahusu vijana, kwa sababu mwandishi Ken Walibora ametilia maanani mabadiliko ya majukumu ya vijana ki-mpito wakati. Zaidi ya hayo, tulishughulikia changamoto ambazo vijana wanakumbana nazo wanapojitahidi kuleta mapinduzi katika jamii.

Nyamemba (2012), alishughulikia uchanganuzi linganishi wa jinsi waandishi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi (2013)* wanavyoshughulikia masuala ya vijana. Alitilia maanani matatizo yanayowakumba vijana kijumla na yale matatizo ya vijana yanayoibuka katika ushairi teule.

Amelinganisha na kutofautisha waandishi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi* kuhusu masuala ya vijana. Pia, amegusia changamoto ambazo zinawakabili vijana. Kazi hii ilitusaidia pakubwa kwa sababu ilishughulikia vijana na changamoto zinazowakumba ambazo sisi pia tulishughulikia. Aidha, sisi tulizingatia zaidi mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko.

Utafiti uliofanywa na Kiongera (2012), ulitufaa sana katika kazi yetu. Mtafiti huyu alionyesha kuwa wahusika vijana ni mawakala wa mabadiliko na wanaweza kufanikiwa katika kuwatetea wanyonge katika jamii. Madai yake yanajitokeza katika tamthilia nne za Kiswahili zilizoandikwa katika karne ya ishirini na moja. Tamthilia hizi ni *Kifo Kisimani* (2001), *Pango* (2003), *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004) na *Seserumbe* (2009). Katika kazi hizi, vijana wamesawiriwa wakiwa msitari wa mbele ili kuleta mabadiliko yanayowafaidi wanajamii wanaodhulumiwa kwa misingi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Katika riwaya tulizozitafiti, vijana wameonyeshwa kama wanajamii waliojizatiti ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Katika kazi yetu tulionyesha changamoto wanazokumbana nazo vijana.

Naliaka (2012), alishughulikia hali ya vijana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara (2007).* Katika kazi yake umuhimu mkubwa umepewa vijana. Alionyesha jinsi vijana wanavyotumiwa kama vipanya vya maabara. Pia, aliangazia matatizo ambayo huwakumba vijana mijini nchini Kenya, mji wa Nairobi ukitumiwa kama mandhari ya riwaya husika. Naliaka ameonyesha kuwa matatizo mengi yanayowakumba vijana husababishwa na wazazi au watu wengine wazima katika jamii ambao wana ushawishi mkubwa katika jamii. Utafiti wa Naliaka ni muhimu sana katika kazi yetu kwa sababu unaonyesha matatizo yanayowakumba vijana kijumla na chanzo cha changamoto ambazo zinawafanya vijana hawa kuleta mabadiliko. Matatizo kama haya ndiyo yanawafanya vijana kuchukua nafasi mbalimbali na kujikomboa katika riwaya ambazo tulizitafiti. Naliaka aliongozwa na nadharia ya uhalisia, na sisi tuliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa.

Dhuluma kwa vijana wa kike ziliangaziwa na Obore (2012). Alisema kuwa suala la dhuluma kwa vijana wa kike linabainika wazi na suala hilo limejitokeza kwa hali mbalimbali na kudhihirisha kuwa vijana wa kike wamekandamizwa na kunyimwa haki. Haya yamesababishwa na kuonekana kwa vijana wa kike kama viumbe duni na wanaume ambao wana msingi na kaida zenye mashiko katika mila na tamaduni zinazopendelea vijana wa kiume. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa sababu umeshughulikia vijana wa kike kwa kuonyesha jinsi wanavyodhulumiwa na kunyimwa haki kwa misingi ya jinsia. Kazi hii hata hivyo, ni tofauti na yetu kwa kuwa sisi tulishughulikia vijana wote wa kike na wa kiume. Pia tulionyesha kuwa vijana wa kike wana uwezo wa kuchangia katika ujenzi wa jamii mpya.

Rono (2013), alichunguza uhakiki wa maudhui na fani katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea (2012),* ambayo ni riwaya mojawapo ya zile ambazo tuliteua. Katika kazi yake, Rono ameonyesha kuwa nchi nyingi katika bara la Afrika zilipata tu uhuru wa bendera ambao haukuleta mabadiliko yaliyokusudiwa kwa sababu uchumi na siasa katika nchi hizi zinaendeshwa na mataifa ya kigeni. Anaendelea kueleza kuwa baada ya uhuru, viongozi waliochukua hatamu za uongozi walijirundikia mali na kukosa kuwajali wanajamii wale wengine. Utafiti huu ulitufaa kwa sababu uliangazia baadhi ya maudhui na mbinu zinazotumiwa kusawiri wahusika. Hata hivyo, sisi tulijikita katika kuangalia wahusika vijana na jinsi wanavyochangia kuleta mabadiliko na changamoto wanazokumbana nazo.

Mayieka (2015), alishughulikia masuala ibuka katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Alisema kuwa masuala ibuka ni mambo halisi yanayoikumba jamii ya kisasa ambayo inapitia mabadiliko mengi. Mabadiliko haya huwa ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidini na kiteknolojia na huathiri jamii katika mawanda yake yote. Kazi hii ilitusaidia sana katika utafiti wetu kwa sababu inagusia mabadiliko ambayo yanatokea katika jamii. Pia, inashughulikia masuala ibuka ambayo huwa ni kati ya changamoto ambazo wanajamii hukabiliana nazo. Changamoto hizi zinaweza kuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya jamii. Katika kazi yetu, tulionyesha jinsi wahusika vijana wanavyojitahidi ili kupambana na changamoto hizi ndiposa jamii ipate kuwa na maendeleo. Katika kazi yetu, tuliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa ambayo ni tofauti na nadharia ya uhalisia iliyotumiwa na Mayieka. Utafiti wa Mayieka ulitufaa sana katika kazi yetu kwa sababu ameshughulikia riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* ambayo ni mojawapo ya riwaya ambazo tumeziteua. Masuala ibuka ambayo ameyashughulikia yalituongoza katika kujadili changamoto za vijana.

Muriithi (2016) alimulika changamoto ambazo huwakumba vijana na akaonyesha athari za changamoto hizi katika riwaya za *Upotevu* (2005) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007). Aliongozwa na nadharia ya uhalisia kuchanganua changamoto hizi, kwani zina uhalisia mkubwa katika maisha ya vijana. Baadhi ya changamoto hizi ni kama vile mapenzi ya kiholela, dhuluma na unyonyaji, utabaka, tamaduni na ufisadi. Utafiti huu ulitufaa sana katika kazi yetu kwa sababu kazi tulizoziteua zimeangazia changamoto hizi. Aidha,

tulionyesha jinsi vijana wanakabiliana na changamoto hizi na kufaulu katika kuleta mabadiliko katika jamii zao.

Ukombozi wa kisiasa na kiuchumi katika riwaya ya *Mkamandume* (2014), ulitafitiwa na Osango (2015), kwa kutumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Alijikita katika maudhui ya kisiasa na kiuchumi kwa kurejelea vipindi vya ukoloni na baada ya ukoloni. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu ilitupatia mwelekeo kuhusu nadharia ya uyakinifu wa kijamii ambayo ndiyo tuliyotumia katika utafiti wetu. Hata hivyo, sisi tulijikita katika mapinduzi yanayosababishwa na vijana.

## 1.8 Msingi wa kinadharia

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Nadharia hii ilituongoza katika kuhakiki jinsi wahusika vijana wanaweza kuangaza uovu katika jamii na juhudi wanazotia ili kukabiliana na uovu huu.

### 1.8.1 Usuli wa nadharia ya uyakinifu wa kijamii

Utafiti huu unahusu uhakiki wa mchango wa vijana katika kuleta mapinduzi katika jamii. Kwa hivyo, nadharia inayofaa ni ile inayohusiana na utetezi wa wanyonge na ukombozi wao katika jamii. Kwa sababu hii tulichagua nadharia ya uyakinifu wa kijamii ambayo iliasisiwa na Stalin mwaka wa 1934, miaka michache baada ya mapinduzi ya Urusi ya mwaka wa 1917. Stalin aliishi miaka ya 1878-1953. Msukumo wake wa kutaka kubadilisha jamii ya Urusi ulichangiwa mno na mawazo ya Maksi hasa alipokuwa mhazili wa Chama cha Ujamaa. Malengo yao makuu yalikuwa kuzindua tabaka la chini la wanaonyanyaswa ili wafahamu na kutetea haki zao dhidi ya tabaka la juu. Stalin alitumia mwongozo wa nadharia ya umaksi ili kuonyesha uyakinifu wa maisha kwa kuleta usawa.

Nadharia ya uyakinifu wa kijamii ilihusishwa na mahusiano ya kitabaka katika jamii yaliyozua mikinzano. Kwa sababu ya maovu, jamii huwa na mikinzano ambayo itamalizika tu iwapo mfumo wa uzalishaji mali utakuwa mikononi mwa mafalahi. Istilahi hii ya uyakinifu wa kijamii ilichangiwa sana na wahakiki wengine baada ya uasisi wake miongoni mwao akiwa ni Lukacs (1963). Lukacs alieleza kuwa uyakinifu wa kijamii una uwezo wa kusawiri jamii katika

ukamilifu wake na kuonyesha hatua za jamii hiyo za kimabadiliko. Pia, alisema kuwa uyakinifu wa kijamii huzingatia hali halisi ya jamii na kuitumia kueleza jinsi jamii inavyoelekea kwenye usoshiolisti. Jamii hupata msukumo fulani ambao huleta mabadiliko hasa wahusika wanapokumbwa na ubaguzi fulani kama vile wa kisiasa, kiuchumi na kisosholojia. Nadharia hii imetufaa katika utafiti wetu kwani masuala yanayogusiwa yanaleta uyakinifu wa maisha.

Bretch (1973) alieleza nadharia hii kuwa ni sanaa ya kimapambano inayopambana na mawazo ya uongo kuhusu hali halisi ya jamii na hisia zinazohujumu maslahi ya binadamu. Nadharia hii pia huangalia hali halisi kutokana na misimamo ya mafalahi na wasomi waliojitolea kuwatetea na wanaopenda usoshiolisti. Kwa mujibu wa nadharia hii, wanyonge basi wanahitaji kutiwa motisha ya kuendelea na mapambano yao ya kujikomboa na kurejesha utu. Hivyo basi, fasihi haina budi kuwapa wanajamii moyo wa kuendelea na mapambano na kusaka ukombozi. Bretch anaamini kuwa jamii itakapozinduka na kupata ukweli wa mambo halisi, itaweza kuleta usawa kwa wote. Hivyo basi alitumia maneno yake kuwa silaha ya ukombozi kwa jamii.

Kimani wa Njogu (1989) anasema kuwa uyakinifu wa kijamii hutetea maslahi ya walio wengi katika jamii na hulenga katika wakati ujao wenye utu na usawa. Dhamira yake kuu huwa ni ukombozi. Ukombozi huu kwa mujibu wa uyakinifu wa kijamii huongozwa na tabaka la wafanyakazi.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa fasihi huwa na sifa bia ambazo huipa sifa za kiulinganishi. Mhakiki huyu anadai kuwa msingi wa fasihi ni binadamu kwa sababu jamii mbalimbali zimeundwa na binadamu. Hii ndiyo sababu kuu ya fasihi kuingiliana.

### 1.8.2 Mihimili ya uyakinifu wa kijamii

Nadharia ya uyakinifu wa kijamii huongozwa na mihimili ifuatayo:

(i) Nadharia hii husawiri jamii katika ukamilifu wake na kuonyesha hatua za jamii kimaendeleo. Huwa na wahusika wa kimaendeleo ambao hunuia kupindua na kuibadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika ambao huwa na nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao. Mhimili huu ulitusaidia kuonyesha jinsi

wahusika vijana walivyojitoa mhanga ili kupambana na uovu katika jamii yao, wakiwa na lengo la kubadilisha hali yao ya maisha ambayo ni duni.

(ii) Wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka pamoja na kusawiri matukio kihistoria. Hufanya hivi kimakusudi au bila kufahamu. Tabaka la wanyonge hujifungata masombo ili kujipa mamlaka na nguvu za kiuchumi. Kwa mujibu wa mhimili huu, jamii katika vitabu viteule, imegawika katika makundi mawili; kundi la wanyanyasaji na wanaonyanyaswa. Pia, matukio yamesawiriwa kihistoria ambapo matukio ya awali katika jamii husika yameonyeshwa.

(iii)Uyakinifu wa kijamii huzingatia hali halisi ya jamii na maslahi ya makabwela ambao ni mafukara wa ulimwengu wanaotaka kuimarisha udikteta wa makabwela. Hutumia hali hii kueleza jinsi jamii inavyoelekea kwenye usoshiolisti. Mhimili huu ulitufaa katika utafiti wetu kwa sababu maslahi ya wanyonge yamezingatiwa. Haya yanadhihirika wakati ambapo vijana wanafaulu katika kubadilisha hali za wanyonge.

(iv) Wahusika huonyeshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza sauti vya watunzi hupulizwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaojua. Katika utafiti wetu, mwandishi amewaonyesha wahusika wake kiyakinifu. Amewapuliza uhai binadamu wa kawaida ambao ni vijana ili apitishe ujumbe wake kwa wasomaji. Kwa hivyo, mhimili huu ulitufaa sana katika utafiti wetu.

(v) Huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu. Hii inamaanisha kuwa mtu atakuwa mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote. Mhimili huu ulitufaa katika utafiti wetu kwa sababu baada ya mapambano, vijana wanatokea kuwa washindi na kuikomboa jamii dhidi ya unyanyasaji.

Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi inapaswa kutumiwa na wanajamii kama kioo ili kumsaidia kuibadilisha jamii yake kutoka katika unyanyasaji na kuleta mabadiliko ambapo kutakuwa na mfumo mzuri wa kuiendeleza jamii bila utabaka.

Nadharia hii ya uyakinifu wa kijamii iliufaa utafiti wetu kwa sababu inaonyesha jamii katika uyakinifu wake ambapo kuna migogoro kati ya mamwinyi na makabwela. Pia inapeana matumaini ambapo wahusika wa kimaendeleo wana uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii na kutupilia mbali utabaka. Riwaya ambazo tulizichunguza zinaonyesha haya yote ambapo kuna migogoro kati ya wanyanyasaji na wanaonyanyaswa na baadaye wanyonge wanafaulu katika kuleta mabadiliko.

## 1.9 Mbinu za utafiti

Uteuzi wa sampuli ambao ulitumiwa katika utafiti huu ni wa mbinu–kusudio. Mbinu hii iliwezesha kuteuliwa kwa riwaya mbili za Kiswahili ambazo zimesawiri wahusika vijana na kuonyesha mchango wao katika kuleta mabadiliko. Riwaya hizi ni *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea,* za Ken Walibora. Kusudi la uteuzi huu ni kuwa, ulionyesha usawiri wa vijana kimpito- wakati.Vilevile, ulichangia sana katika kukuza uchambuzi wa riwaya.

Data ambayo ilitumika katika utafiti huu ilitoka maktabani na mtandaoni. Maktabani, utafiti huu ulihusu kusoma kwa makini na kuchanganua riwaya mbili za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea* ili kuchunguza na kuangazia michango ambayo vijana wametoa katika kuleta mabadiliko katika riwaya hizo mbili. Pia, tulinuia kuonyesha baadhi ya changamoto ambazo vijana wamekumbana nazo katika harakati za kuleta mabadiliko katika riwa za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*. Vilevile, makala na machapisho yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti yalisomwa. Kwa mfano; vitabu, majarida na tasnifu za wasomi wengine. Pia, tulisoma vitabu ambavyo vina maelezo kuhusu nadharia ya uyakinifu wa kijamii, ili tupate kujua misingi ya nadharia hii, mihimili yake na waasisi walioianzilisha.

Huduma za mtandao zilitumiwa ili kupata maelezo kuhusu nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Mbali na kupata maelezo kuhusu nadharia, tuliangalia dhana ya vijana na maelezo mbalimbali ambayo yamejitokeza sana mtandaoni.

Data iliyotokana na usomaji wa vitabu teule ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika jamii ulionyeshwa. Pia changamoto ambazo vijana wanakumbana nazo katika kuleta mabadiliko ziliangaziwa. Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya uyakinifu wa kijamii.

## 1.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia mambo ya kimsingi katika utafiti. Tumetoa utangulizi wa kazi yetu kwa kutoa maana ya neno kijana. Tumeonyesha tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na tukatoa sababu za kuchagua mada. Pia, tumeangazia upeo na mipaka ya kazi yetu. Nadharia ya uyakinifu wa kijamii imeelezwa, yaliyoandikwa kuhusu mada yakaonyeshwa na mbinu za utafiti tulizotumia zikaelezwa.

# SURA YA PILI

# SUALA LA VIJANA NA MABADILIKO KATIKA *KUFA KUZIKANA* NA *KIDAGAA KIMEMWOZEA*

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tulichunguza mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea.* Ken Walibora katika riwaya ya *Siku Njema* (1996) alisema kuwa kitu cha aushi duniani ni mabadiliko kwa sababu mambo mengine yote hufikia kikomo lakini mabadiliko hutokea kila mara na hayafiki ukomoni. Watu wengi katika jamii hawapendi kufumbata mabadiliko yawe chanya au hasi. Hata hivyo, mabadiliko hasa chanya ni muhimu sana na yanapotokea, jamii haina budi kuyafumbata na kuyakubali.

Mabadiliko yanaweza kuwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Watu hutekeleza mabadiliko kwa sababu huwa hawajaridhika na jinsi viongozi wanavyowatawala au kwa sababu ya kuchukia mifumo dhalimu ambayo huwa inadumisha maslahi ya watu wachache wenye mamlaka. Mabadiliko yanaweza kutekelezwa kwa kutumia nguvu au yakapatikana kwa njia ya amani. Vijana wengi katika kazi hii wanatumia amani kutekeleza mabadiliko kama vile baadhi ya majina yao yanaashiria. Mwandishi yeyote yule wa kazi ya sanaa haandiki katika ombwe tupu bali huwa ameshuhudia matukio katika mazingira yake ndiposa anaamua kuyaangazia kwa kutumia wahusika kama kipaza sauti chake.

Vijana katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea* wamesawiriwa kama mawakala wa mabadiliko. Wamejizatiti kubadili mambo ambayo yanaonekana kuzuia maendeleo katika jamii. Mabadiliko haya yanatekelezwa katika nyanja mbalimbali kama vile utawala, imani potovu za kijamii zilizopitwa na wakati, ubaguzi, suala la ufisadi na mitazamo ya watu kuhusu mambo, kati ya mengine. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, vijana wanaochangia kuleta mabadiliko ni kama Amani, Imani, Madhubuti, Mashaka, Lowela, Bob DJ, Benbella, msichana katika matwana na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tandika. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* vijana wanaoendeleza mabadiliko ni kama Akida, Tim, Tom, Jerumani, Pam, Cynthia Tamari na vijana wa Chuo Kikuu cha Kiwachema.

## 2.2 Utawala mbaya na ufisadi

Utawala mbaya huwa unaenda sambamba na ufisadi. Wanajamii wakichagua viongozi wabaya bila shaka kutakuwa na ufisadi. Amani katika *Kidagaa Kimemwozea* aliwaambia wananchi wa Tomoko kuwa kuwapo kwa viongozi wabaya mamlakani si kosa lao tu bali wao pia ni wakosaji kwa sababu ndio huwachagua. Anaendelea kusema kuwa viongozi wakitokea kuwa wafisadi, wananchi ndio huwaruhusu kwa kunyamaza badala ya kuwashutumu viongozi hao. Kijana Amani aliamua kumkabili Mtemi Nasaba Bora kuhusu umiliki wa mali yake.

Baada ya Amani kumwokoa Mtemi Nasaba Bora wakati alipokuwa karibu kuuawa na genge la majambazi, Mtemi alimpeleka Amani nyumbani kwake na kumwambia amwitishe chochote alichotaka. Amani alichukua fursa hii kumdadisi Mtemi kuhusu mali aliyoimiliki. Amani alimwambia:

> ...Halafu naomba unieleze kinagaubaga mali yako umeipataje, mashamba na kadhalika? Nimenunua kwa jasho langu. ``Hukupoka mali ya mtu, hukubini na kughushi chochote na kufanya maskini sina sinani wakiulizwa hawaungami kumaskinika zaidi, waliokuwa na kichache wasiwe na chochote? Hukufanya njama yoyote mtu akauawa na mwingine akafungwa bure? (uk. 148)

Hii ni hatua mojawapo ambayo Amani amechukua ili kuangazia uovu wa kiongozi huyu wa kuwapokonya watu mashamba yao na kuwafunga jela na hata wengine kuuawa. Amani anamwitisha Mtemi Nasaba Bora hatimiliki zote alizokuwa nazo na kuzikagua kwa makini. Aligundua kuwa kulikuwa na hatimiliki mbili tofauti kwa kila shamba, moja bandia na nyingine halali, jambo lililomfanya athibitishe mambo aliyofichuliwa na amu yake Yusufu kuhusu wizi wa mashamba.

Mtemi Nasaba Bora anashangaa vile Amani amegeuka kuwa imara. Hatetereki. Hii ni ishara kuwa hata Mtemi mwenyewe ameanza kuona mabadiliko ambayo Amani ameyaleta. Mwandishi anasema kuwa; "Mtemi Nasaba Bora alishangazwa na vile kijana hariri kama yule alivyogeuka imara kama ukuta wa chuma, hatetereki.''(uk.149 ).

Amani anachukua hatua nyingine ya kuzipeleka hatimiliki alizopata mahakamani kama ithibati. Pia anamwambia Mtemi atoboe siri ya njama zake ndio amu yake aliyefungwa jela aachiliwe. Haya yanamfanya Mtemi kukiri aliyoyafanya, jambo ambalo litaleta mabadiliko kwa maisha ya wengi watakaotendewa haki baada ya ukweli kudhihirika. Mtemi alisema:

> ...kwa kweli najuta, alisema Mtemi Nasaba Bora baada ya kushusha Pumzi. Nilifanya mengi mabaya lakini siwezi kukueleza yote. Katika wizara ya ardhi na makao nilikoanzia ajira niligundua kwamba yupo Mtomoko aishiye nchi ya nje ambaye amenunua shamba la mzungu yaani *special plot.* Niliwalipa majambazi kumumaliza pindi awasilipo nchini. Nilijua fika kwamba mwanawe Yusufu angempokea uwanja wa ndege. Nilitaka kuwamaliza wote lakini watu niliowalipa hawakufuata maagizo vema. Ikawa lazima kutafuta njia ya kumfungisha jela kwa kumnasibisha na mauaji ya babake. Ilibidi kulipa hela nyingi za kadhongo kuwalipa polisi, makarani wa mahakama, majaji, wajua tena mti hauendi ila kwa nyenzo (uk. 150)

Amani hakomi ila anaendelea kumhoji Mtemi na kumtaka kuwataja waliomsaidia kutekeleza njama hii. Hili linamaanisha kuwa waovu wote watachukuliwa hatua na jambo hili litaleta mabadiliko makubwa kwa kuukomesha ufisadi katika jamii. Kwa hivyo, jamii mpya itakuwa imejengwa.

Baada ya mashamba yaliyokuwa yamenyakuliwa na Mtemi Nasaba Bora kutwaliwa, Amani alikuwa mmoja wa wale waliofaidika sana kwa sababu mashamba mengi yalikuwa yamenyakuliwa kutoka kwa nasaba yake. Amani alifanya mabadiliko kwa sababu wengi walitarajia ajiwekee hayo mashamba na kuyatumia na nasaba yake. Kinyume cha matarajio, Amani aliamua kuwafaidi wanajamii wenzake badala ya kujirundikia mashamba hayo. Amani alikumbuka kauli ya DJ kijana mwenzake, walipokutana mwanzo mwanzo huko mto Kiberenge alimwambia; "Lakini *one day* mkilala mafukara mkaamka wadosi msinisahau mwenzenu DJ" (uk. 155).

Alimkatia Bob DJ ekari ishirini na mwenyewe akaendelea kuishi kwenye kibanda chake cha zamani. Aliendelea na kazi zake za sulubu na kila mara kuwazia kuhusu ardhi. Ardhi ndicho kichocheo kikubwa cha unyama wa binadamu.

Kwa kushauriana na amu yake Yusufu, Amani aliamua kulikata shamba tena. Alikata ekari mia moja vipandevipande na kuwapa maskini wa Sokomoko. Ekari hamsini alimpa Madhubuti mwanawe Mtemi Nasaba Bora. Madhubuti naye alichukua ardhi hii na kuigawa yote kwa maskini wa Sokomoko. Kila mtu alimtarajia Amani kuishi kwenye Kasri la Mtemi Nasaba bora. Badala yake, aliinadhifisha kasri hiyo na kuipatia mzee Matuko Weye aliyefikiriwa kuwa mwendawazimu tangu alipopigana vita vya ulimwengu. Amani alisema:

> Alimpigania vita Malkia wa Uingereza. Ni nini alichopewa ila wehu na ukata? Na ni nini Serikali ya Tomoko huru ilifanya kumchonjomoa maskini mzee Matuko Weye? Acha aishi kwenye nyumba hii ya mzungu maadamu angali hai. Tutamtafutia daktari wa akili na wauguzi kumsaidia (uk. 156)

Baada ya Mtemi Nasaba Bora kutoweka, kaimu Mtemi aliteuliwa kushikilia wadhifa wa Mtemi Nasaba Bora. Kaimu Mtemi aliitisha mkutano kuhutubia umma. Kwenye mkutano, umma ulimtaka kijana Amani kuhutubia na ikiwezekana afanywe Mtemi wao mpya. Kinyume na matarajio yao ingawa Amani alitoa hotuba nzuri kupindukia, alikataa kuwa Mtemi. Tunaambiwa kuwa umma ulidai:

> Amani awe Mtemi! Umati ukadai ; hapana. Hata kidogo. Badala yake, acha amani iwe na Mtemi mpya. Msinivishe joho ambalo si makamo yangu kulivaa, aliwaambia. Kaeni mfikirie vema juu ya mustakabali wenu. Nilichodhamiria mimi ni kushirikiana na ndugu yangu Madhubuti kumnyonyoa kipungu mmoja ila sikutaka niingie pahala pake niruke juu nikijihadaa kwamba nitafika mbinguni ... (uk. 157-158)

Amani aliwapatia wananchi ushauri mzuri kuwa wasikubali dhuluma na ikija tena dhuluma wajilaumu wenyewe. Aliwaambia kuwa kuwepo mamlakani kwa Mtemi Nasaba Bora, muda wote huo si kosa lake tu bali kosa lao wote. Walimruhusu wenyewe kwa kimya chao kwa kukubali dhuluma zake kwa sababu ya udhalili wao. Kwa kila mtawala katili kuna umma uliomruhusu ama kumpa uwezo wa kutekeleza ukatili wake. Wananchi walistaajabu kwa sababu ni nadra sana mtu kukataa uongozi na pia hawakutarajia hotuba kama hiyo kutoka kwa kijana kama Amani. Haya yote yanaonyesha kuwa vijana wamejitolea kuleta mabadiliko katika jamii na kusisitiza ujenzi wa jamii mpya kwa kuwazindua watu na kutoa kasumba potovu kwenye akili zao kuhusu uongozi.

Vijana hawa wawili, Madhubuti na Amani walishirikiana na kuangaza uovu wa watawala. Wanajaribu kuchambua maoni ya waandishi wa vitabu na kutambua kuwa viongozi wa baada ya uhuru ni wasaliti wakubwa waliorithi tabia mbaya ya mkoloni mkongwe. Viongozi hawa wana tabia inayofanana ya kumpunja na kumdhulumu mlalahoi.

Madhubuti anatoa mfano wa babake mzazi, Mtemi Nasaba Bora. Anasema kuwa babake ni mfano bora wa hawa wasaliti wanaoteketeza matumaini ya bara zima la Afrika. Madhubuti anasema kuwa Mtemi Nasaba Bora kuwa babake si sababu ya kumfanya afumbie macho udhaifu wake. Anamwambia Amani kuwa amerudi kutoka ng'ambo akiwa na hamasa kubwa ya kuwasaidia wanyonge na kutoa mfumo usiokuwa wa haki na usawa. Ndipo anasema kuwa anataka kuanzia kwao kiamboni alikozaliwa kwa kuangaza maovu ya babake Mtemi Nasaba Bora. Madhubuti anamtaka Amani amsaidie kupambana na uovu huu.

Amani anamwambia Madhubuti kuwa nchi yao haihitaji shahada za vyuo vikuu bali inahitaji shahada kutoka vyuo vya maisha vinavyofundisha watu kuwa binadamu, hasa watambue maadili, haki na usawa. Madhubuti anajuta kwa kufaidi pesa za ufisadi. Anasema kuwa babake angempeleka tu katika vyuo vya humu nchini alipomaliza masomo yake ya sekondari badala ya kupelekwa ng'ambo kwa pesa alizowatoza wananchi kwa lazima. Pia, Madhubuti alikataa kazi aliyotafutiwa na babake kwa njia ya ufisadi.

Mtemi Nasaba Bora alikuwa ametoa hongo ili mwanawe akitoka ng'ambo aajiriwe mara moja. Kinyume cha matarajio ya Mtemi, Madhubuti aliporudi aliikataa kazi hiyo kwa kusema kuwa hawezi kufanya ajira iliyopatikana kwa milungura. Mtemi Nasaba Bora anashangaa na kuuliza: "yu wapi mwanangu mtiifu Madhubuti niliyejikusuru kumpeleka Urusi ili awe mtu bora wa halafu?...karudi mwasi mkubwa badala ya kuwa mwanangu kindakindaki"(uk 120)

Hili tendo la Madhubuti linaonyesha kuwa vijana sasa wamejitolea kuasi maovu ya kijamii hata kama inamaanisha kutengana na nasaba yao ili wajenge jamii mpya yenye haki na usawa. Madhubuti anasema kuwa anataka kujiua kinasaba na kuzaliwa upya asiwe na uhusiano wowote na nasaba ya Mtemi Nasaba Bora. Anasema hivi:

> Nijiue kinasaba kama vile watu wengine humu nchini wanavyopaswa kijiua kikabila na kujiua kitabaka ili nchi ipige hatua za maendeleo. Siku moja nitaandika kitabu kuhusu

> machungu ninayohisi moyoni kwa kuwa mwanawe Mtemi Nasaba Bora. (uk.118)

Baadaye, Madhubuti aliamua kuhamia kibandani kwa Amani ambaye alikuwa mfanyakazi wao, na kuacha kukaa katika kasri ya babake Mtemi Nasaba Bora. Kwa kufanya hivi, Madhubuti na Amani wanabadilisha wazo la utengano na ukosefu wa muafaka kati ya matabaka mbalimbali. Hii ni kwa sababu Madhubuti anatoka katika tabaka la juu naye Amani ni wa tabaka la chini. Jambo hili ni kinyume cha matarajio ya wengi wasioamini kuwa matajiri na maskini wanaweza kutangamana. Tunaelezwa hivi:

> Baada ya siku tatu hivi, Madhubuti aliwaduwaza wazee wake kwa kuhamia kibandani kwa Amani. Bi zuhura alilia kwa shake usiku kucha. Mtemi Nasaba Bora alikula yamini: 'Na asiniite baba tena!' (uk. 120)

Ingawa wazee wa Madhubuti walipinga hatua hii ya Madhubuti kuhamia kibandani kwa Amani, yeye hakurudi nyuma. Hili liliwasaidia kuwa pamoja na Amani na kupata muda wa kutosha kuendelea kupanga mikakati ya kuleta mapinduzi. Tunamwona Amani akimwambia Madhubuti kuwa alikuwa anataka kuleta mapinduzi. Anasema; "Kama nakuelewa ndugu yangu'', alisema Amani hatimaye. "Unataka kuleta mapinduzi" (uk.119)

Amani alipokuwa akimrai Mtemi Nasaba Bora ili ajue chanzo cha mali yake nyingi, kwa upande ule mwingine Madhubuti alikuwa anaendelea kufanya uchunguzi ili naye ajue jinsi babake alivyomiliki mashamba huku na kule, tena makubwa zaidi. Tunajulishwa kwamba baada ya kuhamia kwenye kibanda cha Amani aliishi naye hadi alipoitiwa ajira mjini Songoa. Ajira hii aliipata kwa jasho lake mwenyewe bali sio kwa mikono kurambwa. Madhubuti akiwa mjini Songoa alikuwa akiwasiliana na Amani mara kwa mara kwa barua. Katika mojawapo ya barua hizo alieleza kwamba alikuwa amefanya urafiki na maofisa wa Wizara ya Ardhi na Makao kwa lengo la kutaka kujua jinsi babake alivyoondokea kuwa mmiliki wa mashamba hayo mengi.

Madhubuti na Amani wanaendelea kufanya uchunguzi kuhusu mali ya Mtemi Nasaba Bora na umiliki wake. Baada ya Amani kumkabili Mtemi na kumdadisi kuhusu umiliki wa mali yake, Mtemi alihisi dunia haimweki tena na kuamua kujiua. Aliandika barua na kumwachia nduguye Majisifu. Katika barua hii, alikuwa ameungama dhambi zake zote. Aliorodhesha majina yote

ya watu waliohusika katika njama ya kumwua babu yake Amani, Chichiri Hamadi na kumfungisha amu yake Yusufu jela bila hatia yoyote.

Mwalimu Majisifu alisema sasa yeye ni shahidi na isitoshe alikuwa ameyanasa mazungumzo yake na nduguye Mtemi Nasaba Bora kwenye ukanda kama ithibati nyingine. Baada ya haya kutokea, juhudi za kuanzisha upya kesi ya Yusufu zilipamba moto. Amani na Madhubuti walikuwa katika mstari wa mbele katika jambo hili, wakisaidiwa na Mwalimu Majisifu kukusanya mashahidi ili kufanya utetezi wa Yusufu kuwa thabiti, katika nchi ambayo haki mahakamani ni mchezo wa kubahatisha. Majuma machache baadaye madalali walifika katika nyumba ya Majinuni wakidhamiria kupiga mnada mali ya Bwana Mtemi.

Madhubuti aliposikia kuwa mali ya babake inanadiwa alikuja nyumbani upesi. Alikuwa na stakabadhi zilizoonyesha kuwa haingewezekana kunadi mashamba ya Bwana Mtemi yaliyokuwa yamewekwa dhamana ya mikopo yake mingi, kwa sababu hayakuwa mashamba yake halali. Madhubuti alithibitisha kuwa baba yake Mtemi Nasaba Bora alikuwa ameghushi stakabadhi na kwamba mashamba yote yale yalikuwa na wamiliki halali. Amani pia aliwapa hatimiliki alizotoa kwenye sefu ya Mtemi Nasaba Bora, zilizobainisha wamiliki halali wa mashamba yaliyosemekana kuwa yalikuwa ya Mtemi Nasaba Bora.

Amani tangu hapo alikumbuka ukweli alioambiwa na amu yake Yusufu kuwa hatimiliki halali zilikuwa zimefichwa humo chumbani mwa Mtemi Nasaba Bora. Hatimiliki hizo zilifanana kabisa na zile alizozileta Madhubuti kutoka wizarani. Bidii hii ya vijana hawa wawili ilisababisha mabadiliko chungu nzima kwa sababu haki ilitendeka na wamiliki halali wa mali iliyokuwa na Mtemi Nasaba Bora kurejeshewa mali yao. Vijana hawa wamejitolea kwa vyovyote vile ili kuuondoa utawala mbaya, kama vile majina yao yanavyoashiria.

Jina Madhubuti linamaanisha kuwa imara. Kama lilivyo jina lake, Madhubuti alikuwa imara kuhakikisha kuwa amefaulu katika kutimiza lengo lake la kumtoa babake mamlakani na kuhakikisha kuwa haki imetendeka. Jina Amani linaashiria hali ya usalama isiyokuwa na ghasia. Jina hili ni la majazi kwa sababu Amani anatenda mambo yake kwa utulivu mwingi sana na mwishowe anafaulu. Hii ndiyo sababu alikataa utemi na kusema kuwa anataka amani iwe na mtemi mpya, jambo ambalo liliwashangaza wengi. Pia Amani aliamua kuwapatia maskini mali yake yote na kuendelea kuishi maisha yake ya kawaida na kutimiza msemo

unaosema kuwa kupeana ni moyo si utajiri. Amani anafanya haya yote kwa sababu alitaka amani idumu.

Katika harakati za kukabiliana na utawala mbaya na wenye kunyanyasa wanyonge katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, Imani alikataa kwenda mkutano wa hafla ya kusherehekea sikukuu ya wazalendo. Amani anaporejea kutoka kwa mkutano huo, Imani anamuuliza sherehe zilikuwaje naye Amani akamwambia: "Nilikwambia twende ukakataa." Imani alimjibu Amani hivi:

> Ati mimi nende? Watalazimisha wengine kwenda lakini mimi sendi kwa kheri wala kwa shari. Baada ya wewe kwenda kaja askari mmoja wa Mtemi kaniambia 'ondoka twende' Nikamuuliza kama alitaka nende nishangilie uhuru au niomboleze. (uk .75)

Kukataa kuhudhuria mkutano ni hatua madhubuti iliyochukuliwa na Imani ili kupinga uongozi mbaya wa Mtemi kwa sababu yeye haoni haja ya kuhudhuria mkutano na hakuna cha kusherehekea kwa vile hakuna maendeleo yoyote yaliyofanywa baada ya kujinyakulia uhuru.

Baada ya kurejeshewa mali na mashamba yao, Imani alifaulu kumshawishi nduguye Oscar Kambona maarufu kama Gaddafi na aliyekuwa akimtafuta Mtemi Nasaba Bora ili amuue, aache kumtafuta Mtemi kwa ajili ya kisasi. Alimuasa arejee nyumbani kwao Baraka kwa sababu shamba lao lilishawarudia ili asaidie kumtunza ndugu yao Chwechwe Makweche aliyekuwa hodari kwa mpira zamani. Imani naye alikuwa tayari kurejea kwao shamba mahali walikozikwa wazee wao na ndugu zao wengine. Shamba lao la Baraka walilokuwa wamepokonywa na Mtemi Nasaba Bora lilikuwa lao tena. Haya yote yataleta mabadiliko makubwa kwa sababu vijana hawa watatulia kwao tena na kuendelea na shughuli zitakazoleta maendeleo katika jamii.

Vijana wamejitolea kupambana na masuala ya ufisadi na uovu kijumla katika jamii wakilenga kuijenga jamii mpya ambapo hakutakuwa na uovu. Mashaka alimwambia mjomba wake Mwalimu Majisifu kuwa alikuwa haendi shuleni karibu muhula mzima ilhali walikuwa wakimhitaji sana awasaidie katika matatizo yao darasani. Walizungumziana hivi, Mashaka alipomtembelea mjombake:

> Habari za masomo Mashaka?''Majisifu alimuuliza baada ya kitambo. "Nzuri ila twakuona darasani kwa nadra sana... hatujasoma lolote katika somo la Kiswahili karibu muhula mzima (uk.47)

Haya yanaonyesha kwamba Mashaka alikuwa tayari kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu ambapo walimu wengine hawafanyi kazi ilhali wanalipwa. Kama Madhubuti, Mashaka yuko tayari kuanza na jamaa zake katika kupiga vita ufisadi.

Ufisadi ni jambo ambalo linazuia kuendelea kwa jamii. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, Akida ni mmoja wa vijana ambao wako mbioni kupambana na ufisadi na kuhakikisha kwamba mambo yanafanywa kwa njia inayofaa. Kijana huyu anaonelea kuwa ufisadi ndio hufanya majengo kujengwa kiholela na kusababisha maafa kwa sababu waliopewa kandarasi ya kujenga hawajahitimu vema au kubobea katika kazi hiyo. Akida anapoulizwa angetaka kufanya kazi gani baada ya kuhitimu masomo anasema kuwa angetaka kuwa msanifu ujenzi ndio aondoe hilo tatizo la kuporomoka kwa majengo nchini na kuua watu bure. Tunaelezwa hivi:

> Akida, aliniuliza mwandishi mmoja mwanamke wataka kufanya kazi gani uhitimupo masomo?''ʻNataka kuwa msanifu ujenzi,' nikajibu. 'kwa nini?' 'Nimehuzunishwa mno na visa vingi vya majengo yaliyojengwa na kusanifiwa vibaya katika miji mingi nchini, yakiporomoka na kuwaua watu bure bila kisa. Ili kuondokana na tatizo hilo, lazima wawepo wasanifu ujenzi wengi waliobobea katika fani yao. Nikidhani ufisadi ndio hupelekea kuwepo majengo yasiyofikia viwango vitakiwavyo kujengwa mijini. Mimi siwezi kubadili matamanio kwa sababu ya tatizo la ufisadi. Ufisadi ni roho au pepo iliyomwingia karibu kila mtu nchini. (uk.48)

Akida anashuku kuwa kuna sakata katika mitihani ya kitaifa na haya yanamvunja moyo kwa sababu ni ufisadi unaotumiwa kusahihisha hiyo mitihani na kuwapa wanafunzi alama zisizofaa kwani wana uhusiano wa karibu na wenye vyeo. Mwanafunzi aliyeibuka nambari moja; Regina Kato alikuwa mpwa wa Waziri wa Elimu. Naye Donald Kitenge aliyeibuka nambari mbili alikuwa mtoto wa mfanyakazi wa ngazi za juu katika Baraza la Mtihani ya Taifa (BMT). Hii ndiyo sababu Akida anaonelea kuwa hayo matokeo yalikuwa na walakini anaposema;

"Nilishindwa kujizuia kutuhumu sakata ya namna fulani katika mchakato mzima wa mitihani ya taifa."(uk.51). Udanganyifu ukitokea katika mitihani ya kitaifa ni hatari sana katika nchi. Hii ni kwa sababu wanafunzi watakuwa wakipewa vyeti kuonyesha kuwa wamehitimu lakini wakawa hawana ujuzi wa kutosha. Wanafunzi hawa wakihitimu na waajiriwe katika sekta muhimu huenda wakasababisha maafa. Kwa mfano sekta ya utabibu na ujenzi ambapo watu wanaweza kupoteza maisha yao.

Kijana huyu pia anashutumu wachapishaji kwa kukawia sana na miswada ya watu ambao wameandika kazi zao na kuwapelekea wachapishaji ili waichapishe. Jambo hili linawavunja waandishi moyo kwa sababu hata wengine wanaishia kufa kabla hawajaona nakala za vitabu ambavyo wameviandika. Kwa mfano, babake Akida aliaga dunia kabla ya kuiona kazi yake kwa sababu wachapishaji walikawia nayo sana mpaka akaugua na kufa. Wachapishaji wengine huwa wanakawia na miswada ya watu ili wafanye ufisadi na kuiba hizo kazi na kuzipatia watu wengine wakawa ndio waandishi wazo. Hii ndio sababu Akida anapotumwa na babake kuangalia uchapishaji wa mswada wake umefika wapi anawashutumu hawa wachapishaji anaposema:

> Mgonjwa ndio maana amenituma kwako, nikajibu, Ataka ajue diwani yake itachapishwa lini? Mbona nyie wachapishaji mnakawia sana na miswada ya watu? Kama mswada ni mbaya hauchapishiki rejeshea mwenyewe haraka. (uk.51)

Wakati mwingi viongozi wa serikali huwa wanachaguliwa kwa njia isiyo halali na wanaishia kuiongoza nchi kwa njia isiyofaa. Jerumani anasusia mienendo kama hii na ndiposa anamwambia kijana mwenzake; Akida kuwa amevalia kaptura badala ya suruali ndefu kuashiria kuwa nchi yao ina msiba wa kuongozwa vibaya. Kwa hivyo, kaptura yake anailinganisha na bendera ambayo hupeperushwa nusu mlingoti wakati wa msiba. Anaposema haya, machozi yanamtoka njia mbilimbili kwa sababu ya uchungu alio nao moyoni kuona nchi yake ikitawaliwa na viongozi wafisadi. Anamwambia Akida:

> Utakuwa mtu mzima lini Herr Kipande Madodo? Alijibu. 'Unapaswa kujiuliza Kiwachema twendapi? Kiwachema ni nchi yetu ati. Tuwapeje nyadhifa wafisadi, wabaguzi na wapenda ukabila? Haiwezekani! Ndio maana nasusia kila kitu na badala ya suruali ndefu navaa kaptura. Bendera hupeperushwa nusu mlingoti

> wakati gani?....Sio wakati wa msiba? Suruari kipande hii naivaa kama kwamba bendera nusu mlingoti, ishara ya msiba. (uk.163)

Kumekuwa na uovu ambapo askari polisi wanawaua vijana wa vyuo vikuu katika hali isiyoeleweka. Hii ni sababu mojawapo inayowafanya vijana vyuoni kuendeleza maandamano na migomo wakitetea haki zao na kujaribu kupinga unyama kama huu unaoendelezwa na polisi. Pia wakati wa migomo ya wanafunzi vyuoni kunatokea uovu mwingine wa polisi kuwanyanyasa wanafunzi wa kike kwa kuwabaka wakidai kuwa wanakomesha mgomo. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* tunaangaziwa maovu kama haya yanayotekelezwa na polisi kwa vijana na jinsi vijana vyuoni wanavyojaribu kujitetea ndiposa waukomeshe unyama huu na kuleta mabadiliko katika idara ya polisi. Tunaelezwa kuwa redio ya idhaa ya Kiswahili ya BBC ndani ya basi ilitangaza:

> BBC walisema katika taarifa yao kuwa Chuo Kikuu cha Tandika kilifungwa baada ya polisi kutibua maandamano ya wanafunzi ya kupinga kitendo cha polisi cha kumwua mwanafunzi mwenzao katika hali isiyoeleweka ...Na ukiwa mwanamke wakati wa rabsha ndipo unapotamani ungalizaliwa mwanamume,'alisema yule mwenzake msichana. `Kwa sababu mwanafunzi wa kike ndiye shabaha ya askari polisi mwenye uchu. Sio?' Alisaili mvulana.`Bila shaka leo mimi mwenyewe nimeponea tundu la sindano tu', msichana alisema. (uk.138)

Polisi katika nchi yoyote ile wanapaswa kulinda usalama wa wananchi bila ubaguzi. Hata hivyo, polisi mara nyingi huenda kinyume na haya na hata wakatenda uovu wao wenyewe badala ya kuuzuia kama inavyotarajiwa. Polisi wanapofanya hivi, viongozi wa serikali wanafumba macho na kukosa kufanya jambo lolote ili kuzuia uovu huu. Hii ndiyo sababu vijana wa Chuo Kikuu cha Tandika waliamua kuungana na kujitetea wakati mmoja wao alipouliwa na polisi katika mazingira tatanishi.

### 2.3 Tamaduni potovu zilizopitwa na wakati

Katika jamii kuna imani ambazo ni potovu na huwa zinawafanya wanajamii kurudi nyuma kimaendeleo. Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Imani amejitolea kukiuka na kuvunja imani kama hizi na kuleta mabadiliko ambayo yatawafanya wanajamii kupiga hatua za kimaendeleo. Imani ni msichana ambaye aliamua kuvunja mwiko kuhusu maji ya mto Kiberenge. Ilisemekana

kuwa zamani mgonjwa mmoja wa kifafa alitumbukia na kuzama katika mto huu alipokuwa akioga. Maiti yake ilisakwa lakini haikupatikana. Ilizuka itikadi kuwa kutokomea kwa kifafa yule kulikuwa ishara ya miungu kuwapokonya waja haki ya kuyanywa maji ya mto Kiberenge. Imani wakiwa na kijana mwenzake Amani waliamua kuyanywa maji haya lakini hawakufa kama ilivyotarajiwa. Tunaambiwa kuwa:

> Vizazi vingi baadaye pindi kunywa maji ya mto Kiberenge kulipokuwa tena mazoea, watu Sokomoko walisimuliana kuhusu msichana mmoja aliyekuwa wa kwanza kuvunja mwiko na kukosa kufa kama ilivyotarajiwa na kuwa chanzo cha mtazamo mpya kuhusu mto Kiberenge. Mwiko ulikuwa tena si mwiko (uk.7)

Wanajamii wakiendelea kuthamini imani kama hizi watarudi nyuma kimaendeleo. Imani za kijamii ni muhimu lakini kuna zile ambazo huwa zimepitwa na wakati na hazina budi kutupiliwa mbali. Maji ni uhai na yanaweza kuwa kitega uchumi kwa wanajamii. Kwa hivyo, imani kama hii ya kutotumia maji ya mto fulani itazuia maendeleo. Hii ndiyo sababu vijana hawa wawili waliamua kuvunja mwiko na kuyanywa maji ya mto Kiberenge.

Wakati Akida na wenzake walipofika nyumbani kwa kina Tom kwa mazishi ya babake Tom, kuna mila iliyofanywa ambayo kulingana na Akida, inarudisha watu nyuma. Tunaambiwa kuwa kulingana na mila za Kiwachema, ni lazima mtu ajenge nyumba kwao hata kama amejenga makao mazuri huko jijini. Akida anasema hivi:

> Pembeni mwa kiambo cha Mzee Mangala palikuwa patupu, pahali ilikuwepo nyumba ya aushi ya Tom. Alikuwa kajenga nyumba hiyo kwao kusuluhia desturi ya watu wa kwetu kwamba lazima mtu ajenge nyumbani. (uk.96)

Kujenga nyumba ya aushi kama hii mashambani ni gharama tupu kwa sababu Tom alikuwa akikaa kwa nyumba yake mjini na alikuwa amemjengea babake nyumba yake pia. Kwa hivyo, pesa ambazo alitumia kujenga nyumba ya pili ambayo hakuwa akiitumia angezitumia kujiendeleza au kusaidia wasiojiweza katika jamii. Kwa hivyo, maendeleo kama haya yanazuiwa na imani potovu.

Msichana anayeitwa Cynthia anajitokeza ili kupambana na mila zilizopitwa na wakati, ambazo zinazuia maendeleo katika jamii. Kijana huyu anakataa tohara ya wasichana ingawa dada zake

wote wametahiriwa. Anasema kuwa alisikia kuwa tohara ina madhara mabaya kwa sababu hata wasichana wengine hufa. Anaendelea kusema kuwa rafiki zake wawili walifariki mwaka jana.

Cynthia akisaidiwa na mama yake anaamua kukaidi tendo hili la kuwatahiri wasichana na kukubali mama yake amtoroshe hadi mjini Sangura kwenye kituo cha wasichana wanaokimbia tohara ya lazima. Akida ambaye anafanya kazi kwa akina Cynthia ndiye aliyemtorosha Cynthia usiku kwa baiskeli hadi mjini Sangura. Walisafiri kwa matatizo kwa sababu kulikuwa usiku na baiskeli yao haikuwa na kurunzi. Kukubali kwa Akida kumsaidia Cynthia kutoroka tohara ya lazima ya wasichana ni ishara kuwa amejiunga na kijana mwenzake Cynthia ili kupambana na tendo hili la kinyama ambalo ni mojawapo ya tamaduni zilizopitwa na wakati na ambazo ni hatari kama vile Cynthia anavyoeleza:

> Dada zangu wote wakubwa wametahiriwa. Hata Nana afanyaye kazi Nduchi mjini na ambaye ataolewa hivi karibuni. Zamani nilifikiria ni sawa lakini sasa sitaki. Nasikia kuna madhara. Wasichana wengine wawili walifariki mwaka jana pale ng`ambo. (uk.170)

Tendo hili la ukeketaji wa wasichana lilikuwa likithaminiwa sana katika jamii za kale za Kiafrika. Lilichukuliwa kama kivusho kutoka utotoni kwenda uzimani. Tendo hili huwa na madhara mengi sana kikiwemo kifo. Katika jamii ya kisasa, kuna magonjwa sugu ambayo yanaweza kuambukizwa wakati wanawake wanatahiriwa ukiwapo ugonjwa wa ukimwi. Wasichana wakipatwa na madhara haya hawataweza kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya jamii. Kwa hivyo, jambo hili linapaswa kupigwa marufuku kabisa na wanajamii wote wakiwemo wanaume. Hii ndiyo sababu Akida anakubali kumsaidia Cynthia kutoroka.

Tim anapinga mila nyingine ambayo imepitwa na wakati. Mila hii inasema kuwa mtu hapaswi kutaja jina la baba mkwe. Hii ndio sababu Janelle mke wa Tom, mtoto wa Mangala anapotaja jina la baba mkwe anagutuka na kusema kuwa ameghafilika, na kuomba msamaha. Tim anamwambia kuwa baadhi ya mila zimepitwa na wakati na ni bora zitupwe kwenye kapu la sahau. Janelle ambaye ni mzungu anamwunga mkono Tim kwa kusema kuwa yeye haelewi kwa nini baba mkwe wake hawezi kuishi nao katika nyumba yao ya mjini ilhali ni mjane na hana msaidizi. Inawabidi kuajiri watumishi wa kumsaidia huko shambani. Janelle anasema kuwa hata baba mkwe akifa yeye hapaswi kuiona maiti yake na anaruhusiwa kwenda

matangani baada ya yeye kuzikwa. Tim anasema, ''Baadhi ya mila zimepitwa na wakati. Bora zitupwe kwenye kapu la sahau''. (uk.83)

Baada ya kifo cha Mangala, babake Tom, Tim na Tom wanatofautiana wakati Tim anapomdadisi Tom kuhusu mahali atakapomzika baba yake. Tim alikuwa akimpendekezea Tom amzike babake katika makaburi ya umma jijini kwa sababu huko shambani bado vita vilikuwa vinaendelea na ingekuwa hatari sana kwenda huko kuendeleza mazishi. Tim anapinga tamaduni zinazosema kuwa ni lazima mtu azikwe kwao na kuonyesha kuwa tamaduni hizo zimepitwa na wakati. Tim anasema, ''Mbona usimzike kwenye makaburi ya umma jijini? Desturi hizo zimepitwa na wakati Tom''. (uk.91)

Kinyume na matarajio na fikira za wanakijiji wengi kuwa vijana wakisomea ng'ambo huwa hawarudi nchini mwao, Tom anabadilisha huu mtazamo na kurudi nchini mwake baada ya masomo. Anasifiwa kwa kuwa mzalendo kwa sababu ataendelea kujenga nchi yake. Tunaelezwa,''Kwa hivyo Tom akisifiwa na wote kijijini kwa kuwa mtamaduni. Aidha alikuwa mzalendo kwa kuamua kurejea Kiwachema kuihudumia nchi yake baada ya kuhitimu masomo huko n'gambo''. (uk.81)

Vijana wengine watatu; Pam, Tim na Akida waliendelea kuchangia katika kupinga utamaduni kuhusu tohara ya lazima na tohara ya wanawake. Wanasema kuwa hili ni jambo ambalo linarudisha nchi nyuma isipate kuendelea. Kwa hivyo, ni jambo ambalo linapaswa kutupiliwa mbali. Hii ndio sababu vijana hawa wanalichukia jambo hili na kujaribu kupambana nalo kwa vyovyote vile. Pam alisonya kwa dharau wakati yeye akiwa na vijana wenzake Tim na Akida waliposhuhudia mtu mzima akikamatwa kwa lazima akatahiriwe. Tunajulishwa kuwa kazi sokoni ilikoma ili watu wamsindikize mtu huyo akapate tohara. Hili ni jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo kwa sababu badala ya kufanya kazi, watu wanajishirikisha kwa mambo duni kama kulazimisha mtu kutahiriwa. Kijana Akida anasema kuwa watu hawana uhuru ingawa inasemekana wazalendo walimwaga damu yao ili aondoke mkoloni. Tunaelezwa:

> Na u wapi uhuru usemwao ulipatikana kwa wazalendo kumwaga damu yao ili mkoloni aondoke? Au tuseme jamii ilijipatia

> uhuru wa kumhini mtu binafsi uhuru wake? 'Hii ni dhuluma,'alitamka Pam. (uk.56)

Vijana hawa wanasema kuwa visa vya watu kufedheheshwa hadharani na kulazimishwa kutahiriwa vinasinya. Hii ni kweli kwa sababu hakuna mtu aliye na haki ya kumlazimisha mwingine kutimiza matakwa ya kitamaduni hasa katika enzi hii ambapo watu wameerevuka na kujua kwamba baadhi ya tamaduni zilikuwa za kipuuzi na zimepitwa na wakati. Ni heri zitupiliwe mbali na jamii izingatie mambo yanayoleta maendeleo.

**2.4 Ukabila**

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* vijana wamejitolea kupambana na maovu ya kijamii ambayo ni kizingiti cha maendeleo. Suala la ukabila ni adui mkubwa wa maendeleo kwa sababu watu hawawezi kushirikiana vema kama wanashkilia ukabila. Kwa hivyo, nchi haitaweza kupiga hatua za kimaendeleo kwa sababu daima watakuwa katika vita vya kikabila. Vijana wawili, Akida na Tim ni marafiki wa kufa kuzikana ingawa wametoka katika makabila tofauti. Akida ni Mkanju naye Tim ni Mkorosho. Makabila haya mawili yana uadui mkubwa lakini vijana hawa wawili wameamua kuwa ukabila hautakuwa kikwazo kwao na watashirikiana kuukomesha. Jamaa na marafiki wa vijana hawa wawili wanafanya kila wawezalo ili kuuvunja urafiki wao kwa misingi ya ukabila lakini hawafaulu kwani Akida na Tim ni vijana wenye misimamo thabiti.

Akida na Tim wanasaidiana kwa kila jambo kama ndugu wa toka nitoke ijapokuwa wanatoka katika makabila tofauti. Akida alipofaulu mtihani wake wa taifa wa shule ya msingi, alitakiwa kwenda jiji kuu la nchi ya Kiwachema ili kuzawadiwa na waziri kwa sababu aliibuka nambari tatu katika nchi nzima. Akida hakuwa na jamaa zake huko jijini. Tim rafiki yake aliyekuwa akifanya kazi jijini Tandika na aliyetoka katika kabila tofauti la Wakorosho alikubali kukaa na yeye mpaka amalize shughuli zake jijini za kuzawadiwa. Hii ni ishara kwamba hawa marafiki wawili hawako tayari kuachana kwa sababu ya tofauti za kikabila. Urafiki wao wa kufa kuzikana unawafanya wasaidiane kwa hali nzuri na mbaya. Kwa hivyo, wananuia kuleta mabadiliko katika jamii.

Akida hakuwa anafurahishwa na watu waliozungumza vibaya kuhusu kabila lao na ndipo tunamwona akichukia sana hotuba ya mbunge wao Johnstone Mabende alipohutubia mkutano wa hadhara na kuchochea ukabila. Mbunge wao alisema,"Hatutaki madoadoa hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju.''Mheshimiwa Mabende alishangiliwa...Moyo wangu mchanga ulijawa na uchukivu. Mimi ni Mkanju. (uk.2). Viongozi kama Mheshimiwa Mabende wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuupinga ukabila na kuhimiza wafuasi wao kujiepusha na ukabila badala ya kuuchochea wao wenyewe. Hii ndiyo sababu Akida anachukizwa na kuamua kuwa mstari wa mbele kupambana na jambo hili.

Tamari ni dadake Tim na daima alikuwa akimchukia Akida ambaye ni rafikiye Tim kwa sababu si wa kabila moja na wao. Tamari alianza kumchukia Akida tangu utotoni wakiwa shule ya msingi ya Baraki. Akida anasema kuwa, "Tamari aliniona kama mkia wa mbuzi, kuzaliwa kwangu hasara kwa dunia"(uk. 8 )

Mbali na haya, Tim nduguye Tamari aliendelea kudumisha urafiki wake na Akida bila kujali chuki ya dadake. Akida anaelezea kuwa makabila yao yalikuwa na uhasama wa jadi, kila moja likibeua jingine. Anaendelea kusema kuwa kinyume na hayo, Tim na yeye walikuwa wakiitana 'shemeji' ingawa hawakuwa wameoleana. Tunaelezwa, "kinyume cha yote haya, Tim nami tukiitana shemeji, mtu afasiri atakavyo, kwetu mamoja. Hatukuwa na shaka juu ya dhati ya urafiki wetu. Naam urafiki wa kufa kuzikana hasa. (uk.8)

Urafiki kati ya vijana hawa wawili ulikuwa umekita mizizi kwani ulianza kitambo tangu wakiwa shule ya msingi. Akida anasema kuwa wachokozi walikuwa wengi shuleni lakini Tim aliyekuwa mkubwa wake kiumri kwa miaka mitano aliondokea kuwa mlinzi wake dhidi ya bughudha hizo. Akida anasema hivi:

> Nilikuwa mdogo wake kwa yapata miaka mitano. wachokozi shuleni walikuwa wengi, naye aliondokea kuwa mlinzi wangu dhidi ya bughudha zao. Tuseme Tim alinihurumia tu, akanichukulia kama ndugu yake mdogo. (uk.8)

Vita vya kikabila kati ya Wakorosho na Wakanju vilipozuka, Tamari alikimbilia usalama jijini Tandika mahali kaka yake Tim alikuwa akiishi. Tim alikuwa mwenyeji wake rafiki yake wa kufa na kuzikana Akida, aliyekuwa ameenda jijini kwa shughuli ya kutuzwa zawadi baada ya

kupita mtihani. Tamari alipofika, alipata Akida peke yake kwa nyumba ya kakake Tim. Akida alimkaribisha vizuri lakini Tamari anaendelea kumchukia. Akida anasema kuwa alishtuka kumsikia akimfokea:

> Nyie Wakanju wajinga `Ee! Tamari!' Nilimaka'.``Nyie ni wauaji'',aliendelea kufoka. `Tamari usiseme hivyo tafadhali' nilimtafadhalisha kwa matao ya chini. ``Nenda huko bwege wewe'', alinitupia tusi. ``Mwanzo unafanya nini katika nyumba ya kakangu? (uk.63)

Tim anaporejea anampa pole rafiki yake na wanaendelea kuishi pamoja wakisaidiwa na Pam mpenziye Tim aliyejitokeza kuwa msuluhishi kwa kujaribu kumtuliza Tamari. Hata hivyo, chuki ya Tamari kwa Akida inaendelea ingawa hakufaulu kuwatenganisha marafiki hawa wawili ambao wameamua kuwa ukabila ni lazima uzikwe katika kaburi la sahau.

Mjomba wake Tim ambaye ni Mkorosho hapendi urafiki kati ya Tim na Akida kwa sababu Akida ni Mkanju. Haya yanajitokeza peupe wakati Tim aliamua kumtembeza Akida na kumwonyesha alipokuwa akiishi mjomba wake na jamaa zake. Walipofika nyumbani kwa mjomba wake Tim, mjomba hakuwako nyumbani. Alipofika na kuwapata vijana hawa wawili waliomtembelea, aliwakaribisha vizuri lakini baada ya kugundua kuwa Akida alikuwa Mkanju, alipandwa na hasira. Baada ya mazungumzo machache, Tim alimtambulisha Akida kwa mjomba wake:

> Huyu rafiki yangu ,akasema Tim…``Ni Akida.'' ``Akida ni kabila gani?''Aliuliza mjomba wake Tim. ``Mimi ni Mkanju, nikajibu kwa tabasamu.'' ``Eti Mkanju?'' Alitikisa kichwa na kicheko kikavu nilichokiona cha kishetani.``kwani mjomba kuna nini?'' Aliuliza Tim ``Wakanju" aliendelea yule mzee huku amenikazia macho. Hakuna watu wajinga kama wakanju… (uk.25)

Udadisi huu wa mjomba wake Tim uliwaudhi sana vijana hawa na wote wawili wakaamua kujiondokea kwa sababu hawakufurahia maneno ya mjomba yenye kuchochea ukabila. Tim alimuomba radhi Akida mara tu walipotoka nje ya lango kumaanisha kuwa Tim hakumuunga mkono mjomba wake bali alisimama na rafiki yake Akida kwa sababu hao wawili hawataki ukabila.

Mjomba wake Tim alimfuta kazi Tim alipogundua kuwa aliendelea kuwa na uhusiano na rafiki yake Akida ambaye si wa kabila lao la Wakorosho. Tim alifutwa kazi kwa sababu alihudhuria sherehe ya kuzawadiwa ya rafiki yake Akida. Tim anasema:

> Basi ameniuliza jana nilikuwa wapi. Nikamwambia nilienda kwa sherehe ya kuzawadiwa ya rafiki yangu. Akaniuliza` rafiki yako kabila gani?' Nikamjibu Mkanju. Basi wacha zimpande za kwao.` Eeh! Unafanya urafiki na Wakanju huku unaelewa wanatuua sisi Wakorosho. Unasaliti kabila lako? Unamweka Mkanju nyumbani kwako shauri moyo!' Nikamwambia mimi naamini biblia. Biblia husema adui mpende, usimtende na kisasi mwachie. Muumba. Hebu toka hapa. Nimekufuta kazi...umefutwa kazi kwa ajili yangu? Usijali Akida. Tim alinihakikishia yetu mamoja, ije heri au shari. Siwezi kukulaumu katu. (uk.65)

Tendo kama hili la mjombake Tim ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo kwa sababu badala ya kuendelea kuwaajiri vijana ili wapate kujiendeleza, anaishia kumfuta kazi binamu yake kwa sababu ya ukabila.

Akida ambaye ni Mkanju anaamua kumsaidia Tom ambaye ni Mkorosho na kuendelea kupinga ukabila. Anaonyesha kuwa si lazima mtu awe ametoka katika kabila lako ndipo umsaidie. Wakati vita vya kikabila vilikuwa vikiendelea, baba yake Tom aliuliwa. Aliamua kwamba ni lazima apeleke maiti ya babake huko mashambani akaizike huko kulingana na mila zao. Alikataa kabisa kumzika babake kwenye makaburi ya umma jijini eti kwa sababu vita vilikuwa bado vimechacha huko vijijini. Akida basi alikubali kumsindikiza kwenye mazishi. Mazishi yalipokuwa yanaendelea, Tom na wenzake walishambuliwa na wavamizi na wakamdunga Tom mshale kifuani. Wavamizi hawa walikuwa wameongozwa na Sajini Mapengo ambaye alikuwa askari mkuu jeshini kuonyesha kuwa vita vya kikabila vilichochewa na askari. Sajini Mapengo aliwaamuru wamwache Tom pale na warudi jijini.

Wakiwa njiani, Akida aliamua kurudi na kumwokoa Tom bila kujali hatari ambayo ilikuwa inawakabili. Akida alimwambia dereva amshushe na akarudi. Alimbeba Tom usikuusiku mpaka akafanikiwa kumfikisha hospitalini. Huu ujasiri wa Akida wa kung'ang'ana kumwokoa rafiki yake Tom ambaye si wa kabila lake ni ishara kuwa alikuwa amejitolea kabisa kupinga na kuukomesha ukabila. Wengi wangetarajia kuwa kwa sababu Tim ndiye wa kabila

moja na Tom, angepaswa kumsindikiza kwenye mazishi lakini vijana waliamua kuitoa kasumba hiyo kwenye akili za watu.

Tom alichangia katika kupinga ukabila na kusema kuwa ukabila ni ugonjwa mbaya sana na ilibidi utafutiwe dawa na watu wahimizwe ili wabadilike. Haya yalijitokeza wakati Tom na wenzake walikuwa wakizungumziana wakiwa safarini kupeleka maiti ya babake Tom kwenye hospitali ya Tandika. Tom anasema kuwa ukabila ndio ugonjwa mbaya sana ulioenea kote na inabidi utafutiwe dawa. Tim anashangaa na kumuuliza dawa itatoka wapi. Tom anamwambia kuwa maswali kama, 'Wewe kabila gani?' hayapaswi kuulizwa kwa sababu mtu akikuuliza hivyo anajaribu kupima masafa yanayokutenga naye. Aliongeza kuwa majina na lugha ni mambo mengine ambayo yanaleta usaliti.

Alipendekeza kuwa watu wasipewe majina kama Tom Mangala, kwa vile mtu akisikia Mangala au Sululu atajua kuwa huyo ni Mkanju. Tim alihitimisha mazungumzo hayo kwa kusema kuwa watu wa taifa lao husahau kuwa wote ni ndugu na asili yao ni shamba la Edeni. Njia yao ni moja na hakuna tofauti katika watu wa makabila mbalimbali. Mazungumzo yao yanaonyesha jinsi wanavyochukia ukabila na njia ambazo watu wanapaswa kuzitumia ili kupambana nao. Wao ni mfano mzuri kwa sababu wanashirikiana kusaidia mmoja wao akipatwa na msiba ingawa wanatoka katika makabila tofauti.

## 2.5 Mtazamo kuhusu walemavu

Imani alibadilisha mtazamo wa wengi kuhusu walemavu. Mwalimu Majisifu alikuwa na watoto ambao walizaliwa wakiwa walemavu. Mapacha wa kwanza walitoka udenda mdomoni mfululizo na kwenda haja zote katika nguo zao. Hao wengine nao hawakuweza kutembea. Vijakazi walioajiriwa kuwalea walihitaji kujikaza kisabuni. Imani hakujikaza tu kisabuni. Alikuwa na imani na ndiye mtu wa kwanza kuwaona na kuwatendea watoto hao kama binadamu.

Baba yao alikuwa anawachukia mpaka alikuwa anataka kuwatupa majini. Imani aliwapenda watoto wote walemavu kwa dhati na kuvunja rekodi kwa wema aliowatendea na staha aliyowastahi. Tunaambiwa kuwa kisa cha Imani kilisimuliwa na wengi baadaye; "Naam

walisimuliana kuhusu msichana ambaye pia alipindua mtazamo wa wengi kuelekea watu waitwao walemavu."(uk.7)

Mtazamo chanya wa Imani kuhusu walemavu ulimfanya Mwalimu Majisifu ambaye ndiye alikuwa baba ya watoto wale walemavu kubadili mtazamo wake kuelekea watoto wake walemavu. Majisifu anasema, "Hatuwezi kuwa binadamu endapo hatuwaoni walemavu kama wenzetu. Tutakuwa tumelemaa ulemavu mbaya zaidi kuliko ulemavu." (uk.159)

Mtazamo hasi kuhusu walemavu unajitokeza tena kwenye matwana ambapo Nasaba Bora alikutana na msichana mmoja mzuri ajabu. Nasaba Bora alivutiwa naye kwa urembo wake na akaanza kumtaka awe mpenzi wake. Msichana huyo alimwambia kuwa hilo haliwezekani kwa sababu alijua Nasaba Bora angekimbia baada ya kugundua kuwa alikuwa mlemavu. Haya ndiyo yalitendeka baadaye kwa sababu Nasaba Bora alipogundua msichana huyo alikuwa kiguru; baada ya kushuka kwenye matwana, alishindwa la kufanya na kumhepa. Tunaambiwa kuwa:

> Nasaba Bora alimwambia msichana washuke watembee pamoja mjini. Msichana kainama uvunguni kutoa mikongojo miwili ya kwapani... Ndiposa Nasaba Bora kagundua kumbe banati huyo kiguru...'si nilikwambia? Nilijua ngoma hii itakushinda. Nasaba Bora aliondoka pale baada ya kuomba radhi, haya zimemvaa uso...(uk.101)

Taswira ya kijana huyu imejitokeza ili kuonyesha umuhimu wa kuwaona walemavu kama binadamu wenzetu ndiposa tupate kuwa na maendeleo katika jamii kama vile Imani anavyoashiria. Inaaminika kuwa ulemavu sio udhaifu na kwamba walemavu wakipewa nafasi wanaweza kuchangia sana katika kuleta maendeleo.

### 2.6 Mitazamo ya watu kuhusu maisha

Amani na Imani wanajaribu kubadilisha fikira za vijana wenzao na jamii kijumla kuhusu uhusiano wa vijana wa jinsia tofauti. Wanawafunza kuwa vijana wa jinsia tofauti wanaweza kuishi pamoja na kuheshimiana bila kujihusisha katika mapenzi. Tunaelezwa kuwa:

> Amani alistakimu na Imani katika kibanda chake...kwa siku kadhaa. Imani alikuwa akibaki nyumbani mchana kutwa kukitunza kitoto kile kichanga alichopagazwa Amani...usiku Amani alilala kwenye mkeka mkuukuu uliotandikwa sakafuni akamwachia Imani kitanda chake cha teremka tukaze na kitoto chao cha kupanga. (uk.52)

Heshima kati ya vijana hawa wawili inazidi kuonekana kwa jinsi wanavyobadilisha nguo humo kibandani. Amani anasema hivi:

> Tafadhali Imani, alisema Amani, kafumbe macho nibadili nguo. Imani akafumba macho na kupindua kiti bila neno na kukitazamisha ukutani. Hiyo ndiyo iliyokuwa kawaida yao. Wakati Imani alipotaka kubadili nguo pia ilibidi Amani kugeuka na kuangalia upande mwingine na kufumba macho ama yote mawili. (uk.75)

Heshima kama hii ingeshamiri miongoni mwa vijana na wanajamii kijumla jamii ingesonga hatua kadhaa kimaendeleo. Hii ni kwa sababu tangu Amani na Imani walipokutana ukingoni mwa mto Kiberenge usiku, wamekuwa safarini pamoja na heshima kati yao ndiyo iliwafanya kufaulu katika kuleta mabadiliko makuu katika jamii.

Jerumani aliyekuwa akisomea chuo kikuu huko Ujerumani, kama vile Tom anarudi kwao maisha yanapomwendea mrama na kuanza kuchotea watu maji kwa mkokoteni. Wakati alipoulizwa kama haoni aibu kukokota rukwama alikuwa na mtazamo mzuri sana wa maisha. Anasema kuwa ameona Ujerumani matopasi na wafagizi wakifanya kazi zao kwa kujituma, bila kuonea aibu kazi zao. Anasema kuwa hii ndio sababu watu wanapaswa kufumua mioyo yao na kuifuma upya kwani hiyo ndio siri ya maendeleo. Jerumani anaeleza:

> Aibu ya nini? Mimi si bwana mkubwa wa watu hao wa Sangura. Mimi ni mtumishi ati. Nimeona Ujerumani matopasi na wafagizi wakizifanya kazi zao kwa kujituma. Ndivyo maana tunapaswa kufumua mioyo yetu na kuifuma upya. Hiyo ndiyo siri ya maendeleo. (uk.156)

Jerumani anaendelea kumwambia Akida kuwa tunapaswa kuaibikia ukabila bali sio makabila yetu. Anaonya kuwa tunapaswa kutumia dini ili kutugeuza mioyo, bali dini isitumiwe kama mahali pa kujificha na kuwaangamiza wengine. Jerumani anamwelezea Akida kuwa makasisi Wakorosho waliwatesa watu waliokimbilia usalama makanisani huko Korosho. Nyumba za

makasisi ndizo zilizokuwa mabohari ya bunduki, nyuta na mishale ya kuwamaliza watu Korosho. Haya ni mambo kama yale yaliyokuwa Rwanda ya wanadini kusahau dini na kuwaua wanadini wenzao kwa sababu za kikabila. Kwa hivyo, kulingana na Jerumani, watu wanapaswa kuchukua mtazamo mwingine na kubadili mioyo yao kwani kuna mizozo mingi na migawanyiko makanisani, mahekaluni na misikitini.

Jerumani anasema kuwa nchi yao inahitaji mapinduzi. Sio mapinduzi ya serikali bali mapinduzi ya mitazamo au misimamo na mikabala. Anasema kuwa msimu wa tohara ukifika kutakuwa maajabu wasichana watakapokuwa wakilazimishwa kutahiriwa na wengine watoke damu mpaka wafe. Anaarifu kuwa mwaka jana walikufa wawili. Anaendelea kusema kuwa hizo mila ni upuuzi na ndio maana nchi inabaki nyuma. Anasema:

> Hii nchi yetu inahitaji mapinduzi. Sio mapinduzi ya serikali. Hata kidogo. Tunachohitaji ni mapinduzi ya mioyo. Mapinduzi ya ada na mila. Mapinduzi ya mitazamo, misimamo na mikabala...Aisee sisi wanakiwachema tumelemaa vibayavibaya. Subiri msimu wa tohara ufike uone maajabu... utawaona wasichana maskini wanalazimishwa kutahiriwa burebure. Wengine watapatwa na 'blutung' watoke damu wafe. Mwaka jana wamekufa wawili. Lo! Mila gani hizo upuuzi. Ndio maana tunabaki nyuma. (uk.154)

Tamari ambaye ni dada yake Tim na aliyekuwa akimchukia Akida, anabadili mtazamo wake wa maisha na kuacha kumchukia Akida. Tamari anamwomba msamaha Akida na kumwahidi kuwa ametupa jongoo na jiti lake. Ameamua kusahau yaliyopita na kuganga yajayo. Akida anasema hivi, ''Tamari alisema kama kurumbiza. Hisia zetu kuelekeana zilipata mapinduzi makubwa. Kwake sasa nimeingia orodha ya watu. Hahisi kitefutefu tena anionapo.'' (uk.117)

Vijana wakisameheana na kuamua kushirikiana ni ishara kuwa watafanya kazi pamoja na kuleta maendeleo. Vijana ni watu wenye maarifa mapya na nguvu ya kutenda kazi. Kwa hivyo, wakishirikiana wote wataweza kupambana na maovu katika jamii na kuleta maendeleo. Wakati ambapo Tamari alikuwa akimchukia Akida, hakukuwa na amani katika nyumba ya Tim ambapo vijana hawa watatu walikuwa wakiishi. Hata hivyo, kwa sababu ya ushirikiano na urafiki wa dhati kati ya Tom na Akida, Tamari hakuweza kuwatenganisha. Hii ndiyo sababu mwishowe Tamari anaamua kuwaunga mkono Tim na Akida kwa kuacha kumchukia Akida.

## 2.7 Wizi wa miswada

Amani ambaye ndiye alikuwa mwandishi halali wa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, alimwuliza maswali Mwalimu Majisifu kuhusu uandishi na wizi wa mawazo. Walikuwa wakizungumziana na Mwalimu Majisifu wakati walikutana karibu na mto Kiberenge. Majisifu anasema alikumbuka vizuri mazungumzo yaliyomshitua kwa vile kijana aliyefikiriwa hajui kusoma na kuandika alivyoonekana kuangusha hoja nzitonzito na kuuliza maswali kama wakili aliyetopea. Tunaelezwa hivi:

> Hebu nikuulize swali moja, ukiandika kitabu kikawa maarufu ukaambiwa hukukiandika utasemaje? 'jibu mwafaka kwa madai kama hayo ni kunyamaza', alijibu mwalimu majisifu... Lakini ni kweli kwamba upo pia wizi, wizi wa mawazo, wizi wa miswada kama vile ulivyo wizi wa mashamba na magari, wizi wa mitihani na mifugo, wizi wa wake na waume za watu na kadhalika? (uk. 96-97)

Maswali kama haya anayoulizwa Mwalimu Majisifu na Amani yanalenga kubadilisha huo uovu wa mtu kuandika mswada wake na ukaibiwa na mtu mwingine, kama vile Mwalimu Majisifu alivyokuwa amemwibia Amani mswada wake. Jambo kama hili la kuibiwa mswada linarudisha nyuma maendeleo na kuwafisha moyo waandishi wa baadaye kwa sababu wakijua kuwa wataandika na miswada yao iibiwe, hawatakuwa na ilhamu ya kuandika tena. Hili linawafanya vijana kuinuka na kutetea jambo hili.

Mashaka na mjombake Majisifu walipokuwa wakizungumziana, waligusia uandishi wa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* ambayo Mwalimu Majisifu alikuwa anadai kuwa ndiye aliyeiandika. Maswali ambayo Mashaka anamwuliza amu yake kuhusu uandishi wa riwaya hii na jinsi Majisifu anavyoyajibu yanaelekea kuonyesha kuwa Majisifu hajui chochote kuhusu uandishi wa riwaya hiyo. Haya yanafunua uovu ambapo watu huwaibia wengine mawazo na miswada yao. Mashaka alimuuliza amu yake hivi, "Basi *Kidagaa Kimemwozea* kilichukua muda gani kuandika?''Siku moja."Aha! Kurasa zote hizo?''

Mwandishi bora lazima aandike haraka kabla mawazo hayajayeyuka na kugeuka upepo" (uk.48) Katika mazungumzo haya, ukweli kwamba Mwalimu Majisifu siye aliandika kitabu hiki unaendelea kudhihirika.

Wakati Mwalimu Majisifu alikuwa amealikwa kwenda kuhutubia umma huko Wangwani, vijana wa chuoni walimwuliza maswali kuhusu uandishi wa riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea* ambayo ilimfanya kupata umaarufu sana. Mwalimu Majisifu alishindwa kuhutubia *hadhira na hata akashindwa kujibu maswali ambayo alikuwa anaulizwa na vijana* kuhusu uandishi wake. Tunaambiwa kuwa:

> Ghulamu mweusi ti aliamka na kuuliza, 'Mwalimu Majisifu riwaya yako umeiita *Kidagaa Kimemwozea.* Je, unaweza kutuelezea kilichokufanya kuchagua kichwa hicho?' Kwa kweli ee, sijui kwa nini nilichagua kukiita kitabu hicho *Kidagaa Kimemwozea.* Niligutuka tu nimekiita hivyo. (uk.123)

Banati mmoja naye alijitokeza na kuendelea kumwuliza Mwalimu Majisifu maswali kuhusiana na maudhui yaliyomo katika riwaya yake:

> Una maoni gani mwenyewe juu ya jinsi nchi huru za Afrika zilivyo baada ya kuondoka kwa mkoloni? Aliuliza banati mmoja. Ahaa. Kusema kweli Afrika imepiga hatua kimaendeleo baada ya uhuru...kuna umoja na utangamano humu barani... Afrika imejikomboa kutoka matatizo ya njaa. Lakini Mwalimu Majisifu, alidakia tena yule banati kwa nini maoni yako ni tofauti na maudhui katika riwaya yako ya *Kidagaa Kimemwozea* maana huko umeonyesha kuna walakini katika Afrika huru. Sina haja kuzungumzia hapa udhaifu mkubwa wa kimuundo ulio dhahiri shahiri katika riwaya yako. Huo, hata mtoto wa shule ya msingi anaweza kuutambua mara moja. (uk.124)

Kijana mwingine aliendelea kumwuliza Mwalimu Majisifu maswali ili kudhihirisha udhaifu wake. Alimwuliza:

> Je wewe ndiye uliyeandika *Kidagaa Kimemwozea*? Ghulamu mmoja mwenye nywele za rasta aliuliza. Twasikia tetesi kwamba hukuandika riwaya hiyo, kwamba uliuchukua mswada wa mtu mwingine? Mwalimu Majisifu akaubana. Hayo yalikuwa mno. (uk.125)

Haya maswali yanayoulizwa na vijana na jinsi yanayojibiwa vibaya vibaya na Mwalimu Majisifu yanaonyesha. kuwa vijana wamejitolea kuleta mabadiliko katika uandishi kwa

kuwaangazia waandishi bandia ambao wanaiba miswada ya wengine na kuifanya yao. Kwa hivyo, wanachangia kuangamiza wizi wa kitaaluma.

## 2.8 Unyanyasaji wa wanyonge

Katika jamii huwa kuna wanyonge ambao wakati mwingi wananyanyaswa na kuhukumiwa bila hatia. Watu kama hawa wanaweza kuumia sana kama hakutakuwa na mtu wa kuwatetea. Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Lowela alijitokeza na kuamua kuwatetea vijana wenzake; Amani na Imani wakati walipofungwa jela na Mtemi Nasaba Bora bila hatia, ingawa alikuwa mpenzi wake Mtemi. Katika barua aliyomwandikia Mtemi, Lowela alimwambia, "Usipowaachilia wale vijana wawili, mchunga wako na yule msichana waliojisabilia kumtunza mtoto uliyempagaza mchunga huyo nitatoboa siri." (uk.106)

Tendo hili la Lowela ni ishara kuwa vijana wako tayari kupambana na uovu wa viongozi hata kama wana uhusiano wa karibu nao, kama vile Lowela alivyofanya alipomshutumu Mtemi ingawa walikuwa na uhusiano wa kimapenzi.

Amani na Imani walipofungwa gerezani, Bob Dj alikuwa mmoja wa waliojitolea kuwatetea kwa sababu hawakuwa na hatia. Walikuwa wanasingiziwa tu kuwa walikiua kitoto Uhuru. Mtemi anasema kuwa alipokutana na Dj mjini, alimuuliza kwa nini hawezi kuwaachilia wale vijana, Amani na Imani ilhali hawana hatia. Haya yanaonyesha kuwa Dj alikuwa anawatetea vijana wenzake. Tunaelezwa hivi:

> Yule kijana asemaye kama mkora? Mtundu wa mwisho. Kama kaumwa na mbwa, hiyo ni stahili yake. Juzi tulikutana mjini akaniuliza eti kwa nini siwezi kuwaachilia wale vijana kumbe wanaitwaje vile? Amani na Imani… basi kanikuta juzi na kuniuliza kwa nini nisiwaachilie ilhali hawana hatia. Nikamwuliza kama hawana hatia yeye ajuaje. Akanijibu kwa takaburi kwamba na mimi najuaje kama wanayo hatia.( uk.104 )

## 2.9 Umuhimu wa haki za watoto

Kila mtoto anapozaliwa huwa ana haki ya kuishi. Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Mtemi Nasaba Bora na Lowela walikiuka haya wakati Lowela alipojifungua na wakaamua kumtupa mtoto huyo. Amani na Imani wanazindua jamii kuhusu umuhimu wa haki za watoto kwa kujisabilia kukilea kitoto Uhuru ijapokuwa kitoto hiki si chao. Mtoto Uhuru alikuwa amezaliwa na Lowela ambaye alikuwa hawara wa Mtemi Nasaba Bora. Kwa sababu Lowela hakutaka wazazi wake wajue amezaa, naye Mtemi Nasaba Bora hakutaka bibi yake Bi. Zuhura ajue kuwa ana jicho la nje, Mtemi aliamua kumwacha mtoto huyo mlangoni mwa kibanda cha mchunga wa mifugo wake, Amani. Amani aliamua kumwita Imani aje amsaidie na wakamlea mtoto huyo vizuri sana mpaka alipougua na kufariki. Kwa kufanya hivi, vijana hawa wanaonyesha umuhimu wa haki za watoto na kuzitetea.

## 2.10 Kisasi na msamaha

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Amani alibadilisha mtazamo wa wengi kuwa mtu akikukosea ni lazima ujitenge naye na kuacha kushirikiana na yeye. Baada ya Amani kufunguliwa kutoka Jela ambako Mtemi Nasaba Bora alikuwa amewafungia bila hatia, hakuacha kufanya kazi kwake. Ingawa Imani alikuwa anamshawishi aache kufanya kazi kwa Mtemi Nasaba Bora alikataa katakata. Tunaelezwa kwamba:

> Amani alirejea kwake kibandani na kuendelea na kazi ya kuchunga na kukama ng'ombe. Alikataa katakata rai ya Imani kuacha ajira kwa Bwana Nasaba Bora na kutafuta kwingineko. (uk.110)

Kuendelea kufanya kazi kwa Mtemi Nasaba Bora ndiko hasa kunafanya Amani kutambua maovu ya Mtemi na baadaye mabadiliko mengine mengi yakatokea. Pia, licha ya kuwa Mtemi Nasaba Bora alikuwa akiwatesa watu, Amani alisisitiza kuwa Mtemi azikwe kwa heshima kuonyesha kuwa yeye alikuwa na mtazamo tofauti kuhusu watu waovu. Tunaambiwa, "Amani alisisitiza kwamba sharti azikwe Mtemi kwa heshima inayomstahiki si hoja kafanya makuruhu mangapi alipokuwa mamlakani." (uk 159)

Amani alimsamehe tena Mtemi Nasaba Bora kwa kumtandika kinyama baada ya kumpata katika chumba chake cha kulala alipokuwa ameitwa na Bi. Zuhura amsaidie. Mtemi aligundua kuwa Amani hakuwa na ngoa naye baada ya Amani kumwokoa alipokuwa amevamiwa na majambazi njiani. Amani alimwambia Mtemi kuwa ijapokuwa alimtendea maovu, yeye hakumchukia. Anamkumbusha kuwa hali yake ilikuwa karibu sawa na ile ya Yusufu na Potifa. Amani alimsamehe Mwalimu Majisifu baada ya kugundua kuwa ndiye alimwibia mswada wake. Amani aliamua kumwandikia Majisifu ujumbe mfupi wa kishairi na kumwambia kuwa hakuwa na kinyongo na yeye. Ingawa alimwibia utungo wake, anastahili kusamehewa. Amani angeamua kulipiza kisasi huenda hangefaulu katika mapambano yake dhidi ya utawala mbaya. Hii ni kwa sababu watu ambao aliwasamehe ndio wanamsaidia kupambana na uovu.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, Tim anajaribu kubadilisha mtazamo wa vijana wenzake kuhusu kisasi. Anawaonya dhidi ya kujilipizia kisasi kwa kuwaambia kuwa kisasi hakiwezi kujenga nchi. Haya yalitokea wakati vijana wanne walijitoma kwenye chumba cha Tim wakimtafuta Akida wamuue kwa sababu alikuwa amemjeruhi baba yao kimakosa na sasa mahakama ilikuwa imemwachilia Akida kwa kosa hilo. Walikuwa wameamua kumsaka Akida ili walipize kisasi kwani walidai mahakama haipaswi kumwachilia Akida. Huu ndio wakati Tim anachukua nafasi na kuwaambia; ''Umeona wapi kisasi kimejenga nchi?'' (uk.204)

## 2.11 Hitimisho

Katika sura hii tumeangazia kwa undani mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika jamii kwa kuchunguza riwaya ya *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*. Ni wazi kuwa mwandishi wa riwaya hizi mbili ameshughulikia mchango ambao vijana wanatoa katika jamii zao ili kuzibadilisha na kuleta maendeleo. Kwa hakika uhalisia wa kijamaa unadhihirika wazi pale ambapo vijana wanatambua mambo ambayo yanaathiri jamii na kuzuia maendeleo na kujitahidi ili kupambana na mambo hayo.

Masuala ambayo vijana wamejitolea kuyashughulikia katika sura hii ni kama vile utawala mbaya na ufisadi. Vijana kama Amani, Imani, Madhubuti, Mashaka na vijana wa chuo cha Tandika wako mstari wa mbele kuhakikisha kuwa uovu huu umeisha kabisa. Juhudi zao zinaonekana pale ambapo wengine wanaamua kuwashutumu watu wa familia zao. Kwa mfano,

Mashaka alimkashifu Mwalimu Majisifu ambaye ni mjomba wake kwa kutowafunza vizuri. Madhubuti alithubutu kwenda kinyume na baba yake Mtemi Nasaba Bora ambaye alikuwa kiongozi mbaya na mfisadi. Juhudi za vijana hawa zinazaa matunda kwa sababu wanafaulu katika kupambana na ufisadi na kuwaondoa viongozi wabaya mamlakani.

Tamaduni potovu ambazo zimepitwa na wakati ni suala lingine ambalo vijana wamefaulu katika kupambana nalo. Imani, Amani, Akida, Tim na Pam ndio vijana waliojitolea kupambana na jambo hili. Ukabila ambao ni adui mkubwa wa maendeleo unakabiliwa na Akida na Tim ambao walikuwa marafiki wa kufa kuzikana, wakisaidiwa na Tom, ambaye alikuwa wa tabaka la juu kuwaliko. Vijana hawa waliweka kando tofauti zao za kikabila na kitabaka na kuamua kupambana na ukabila bila kutetereka na mwishowe wakafaulu. Watu wengi katika jamii wamekuwa na mtazamo hasi kuhusu walemavu na kuwaona kama watu wasio na haki ya kuishi. Imani na mrembo aliyekuwa mlemavu kwenye matwana moja waliyosafiria na Mtemi Nasaba Bora wanatetea walemavu na kuonyesha wanajamii kuwa ulemavu si udhaifu. Walemavu wakipewa nafasi na kutunzwa vema wanaweza kuishi kama binadamu wale wengine na kujitegemea maishani.

Mitazamo mibaya kuhusu maisha inaweza kuwafanya watu kukosa matumaini maishani. Jambo kama hili linaweza kuwazuia wanajamii wasiweze kutia bidii ili kuleta maendeleo. Katika sura hii, tunaona vijana kama Jerumani na Tamari wakiwahimiza wanajamii wabadili mitazamo yao kuhusu maisha na pia Tamari mwenyewe akabadili mtazamo wake. Vijana wanapotia bidii ili kujiendeleza wanaweza kurudishwa nyuma na watu ambao wanangoja wengine wafanye kazi halafu wawaibie. Jambo kama hili linajitokeza wakati Amani alipoandika mswada wake na Mwalimu Majisifu akauiba. Vijana wanajitokeza ili kumtetea kijana mwenzao kupambana na uovu huu. Kwa mfano, vijana wa Chuo Kikuu cha Wangwani na Mashaka. Haya ni baadhi ya masuala ambayo yameshughulikiwa katika sura ya pili na jinsi vijana wanakabiliana nayo ili kuyabadilisha.

# SURA YA TATU

# CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA VIJANA KATIKA HARAKATI ZA KULETA MABADILIKO KATIKA *KUFA KUZIKANA* NA *KIDAGAA KIMEMWOZEA ZA* KEN WALIBORA

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, tulishughulikia changamoto ambazo huwakumba vijana katika juhudi zao za kuleta mabadiliko kwa kurejelea riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*. Changamoto hizi zinatokana na vijana wenyewe na pia wanajamii wengine ambao hutangamana na vijana hawa. Mwandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea*, ameibua baadhi ya changamoto ambazo vijana wanakumbana nazo katika juhudi zao za kuibua mabadiliko katika jamii yao.

## 3.2 Ulemavu

Fasiri ya neno ulemavu hutofautiana kutoka kwa mtaalamu mmoja hadi mwingine, kutegemea mazingira ambamo fasiri hiyo hutumika. Baadhi ya wataalamu husema kuwa ulemavu ni ukosefu wa viungo muhimu katika mwili wa binadamu huku wengine wakisema ulemavu ni ukosefu wa fikra. Watu walemavu ni miongoni mwa makundi ya watu katika jamii wanaokabiliwa na changamoto nyingi. Changamoto kuu ni ukosefu wa fursa ya kuwawezesha kuishi maisha ya ustawi.Tatizo kubwa linatokana na kubinywa kwa haki zao za kimsingi. Jambo linaloweza kuwasaidia kupata haki zao nyingine ni haki ya kupata elimu. Pindi wapatapo fursa hii ya kupata elimu, haki zao nyingine zote watazifikia kwa urahisi sana kama watu wengine.

Katika dunia ya sasa elimu ni nyenzo muhimu ambayo inampa mtu nafasi ya kupambana na changamoto za maisha kama vile umaskini. Nyenzo hii inamwezesha mtu kubadilika kifikira na hivyo kuleta mabadiliko chanya katika maisha yake na hata jamii kijumla. Kwa hivyo, kila mtoto aliyefikisha umri wa kwenda shule ana haki ya kupata elimu bila pingamizi yoyote. Hata hivyo, walemavu hawapati elimu itakayowawezesha kujitegemea. Nafasi yao ya kupata elimu inakuwa finyu kwa sababu ya mambo mbalimbali. Kwa mfano, wazazi na walezi wa watoto walemavu wanawanyima watoto hao haki yao ya kupata elimu. Kwa sababu za kihistoria mila na

utamaduni potofu, ulemavu umekuwa ukichukuliwa kama balaa katika familia. Kutokana na mapokeo hayo, familia zenye watoto walemavu zimekuwa zikiwaficha watoto hao kwa kuhisi kuwa kuwepo kwa mtoto mlemavu katika familia ni laana. Hali hii imewafanya watoto hawa kukosa haki ya kupata elimu.

Jambo lingine linalosababisha baadhi ya watoto walemavu kukosa fursa ya kupata elimu ni mfumo wa elimu uliopo. Katika taasisi nyingi za elimu kuna miundombinu ambayo ni hafifu na isiyoambatana na hali halisi ya ulemavu. Kwa mfano, vyoo, madarasa na vyombo vya kujifunzia haviwezi kutumiwa na walemavu kwa urahisi. Baadhi ya changamoto hizi zinazowakabili walemavu zimeangaziwa katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Mwalimu Majisifu na bibi yake Dora walikuwa wamepata watoto wanne ambao wote walikuwa walemavu, jambo ambalo halikumfurahisha baba yao Mwalimu Majisifu. Alichukulia jambo hili kama laana na ndio sababu aliwaita masimbi na kuona kama hawafai kuishi. Hata alikuwa karibu kuwatupa majini wafe lakini mkewe Dora akamzuia. Tunaelezwa yafuatayo:

> Mwalimu Majisifu hakuwa mgumba wala mkewe Dora hakuwa tasa. Lakini walijiona wazazi wa laana. Mwalimu Majisifu hasa ndivyo alivyoamini. Walikuwa na watoto wanne; mapacha wale wawili wachanga na watoto wengine wawili, mvulana na msichana. Msichana alikuwa na umri wa miaka kumi na saba naye kamzidi mvulana kwa mwaka mmoja. Hawa wawili wakubwa waliwapa Majisifu na Dora dhiki nyingi kuwatunza. Walitoka udenda mdomoni mfululizo na kwenda haja zote kubwa na ndogo katika nguo zao. Vijakazi walioajiriwa kuwatunza walihitaji kujikaza kisabuni (uk.30)

Ingawa umri wa watoto hawa ni wa kwenda shuleni, wazazi wao hawakuwapeleka shuleni kusoma eti kwa sababu walikuwa walemavu. Dora alipojifungua tena, alizaa mapacha. Hawa nao walizaliwa bila uwezo wa kutembea na Mwalimu Majisifu akataka kuwatupa majini. Hawa pia hawakupelekwa shuleni kwa sababu wazazi wao waliamua kuwafungia chumbani ili wasionekane na watu. Wageni walipobisha hodi mlangoni, Dora aliwafungia hao watoto kwanza kabla ya kufungua mlango. Tunaelezwa:

> Mwalimu Majisifu alijizoazoa na kuketi kochini kiungwana. Kabla ya kufungua mlango, Dora aliwafungia watoto wale afkani katika chumba chao. Akakimbia bafuni na kuja na raka kuukuu alilopangusia mkojo uliokuwa sakafuni sebuleni. Akaizamisha huzuni na hasira yake moyoni na kuvaa uso wenye bashasha ya ghafla. Akaufungua mlango. "Karibu ndani", alimwambia mgeni. (uk. 45)

Tabia ya wazazi na walezi kuwafungia walemavu na kuwanyima haki ya kupata elimu ambayo ni haki ya kimsingi inakuwa changamoto kubwa. Walemavu ni binadamu na wanahitaji kutangamana na watu wengine, kusoma na kupata huduma zote za kijamii katika maisha yao kama binadamu wengine. Walemavu wakiwezeshwa wanaweza kujitegemea wao wenyewe.

### 3.3 Uyatima

Vijana wanapofiwa na mzazi au wazazi wanaweza kupatwa na matatizo ambayo yanaweza kuwafanya wasijiendeleze na hata wasiendeleze jamii zao. Baadhi ya matatizo haya ni kama ukiwa, ambao huwafanya kuwakumbuka wazazi wao daima. Pia, vijana wanaachiwa majukumu ya kuitunza familia ambayo yangetekelezwa na wazazi wao kama wangekuwa hai. Baadhi ya majukumu haya huwalemea vijana kwa sababu ya umri wao mdogo na kuwafanya wasijiendeleze. Baadhi ya changamoto zinazowakumba vijana baada ya kufiwa zimejitokeza katika *Kidagaa Kimemwozea* na *Kufa Kuzikana.*

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* Amani alifiwa na wazazi wake wote na akaanza kuteseka. Baba yake Amani alikufa kutokana na maradhi na kumwacha chini ya ulinzi wa mamake. Mamake Amani naye alikufa baada ya muda mfupi katika ajali ya barabarani na kumwacha Amani akiwa na umri wa miaka ishirini. Baada ya kifo cha mamake, Amani alijawa na huzuni nyingi na kila mara alipomkumbuka, machozi yalimtiririka. Tunaelezwa kuwa:

> Maskini baba mtu kajifia kwa maradhi kabla ya mauaji ya babu… Amani aliyekuwa mtoto wa pekee alihamia ulitima na mamake mjane alikokulia na kulelewa. La, mama mtu hakuwa mkwasi wa kutajika bali pia hakuwa maskini

> mwenye hali ya mkunga, akijikuna hutoka unga. Alikuwa wa sitara hasumbuki wa mbili havai moja. Ndivyo alivyobaki hadi alipofariki kwa ajali ya barabarani, Amani alipokuwa na umri wa miaka ishirini. Amani amdhukurupo mamake mzazi machozi humdondoka (uk.33)

Amani alikuwa akitumainia kwamba mambo yakimtengenea yakawa taibu ataandika mswada mzima wa kitabu kuhusu mamake. Usiku mmoja akiwa kibandani alimoishi alizidiwa na jakamoyo, ikampandisha ilhamu. Alitumia mwangaza wa taa yake ya kibahaluli kutunga shairi fupi kwa heshima ya mamake:

Mkono umeniacha, mwanao kindakindaki
Jitimai imechacha, Amani sifarijiki
Nahisi lau machicha, thamani sithaminiki
Maskini kutwa kucha, natamani kufariki
Tukutane kuko huko
Ulivyonipenda mama, lolote kuniridhia
Ukajisimamia wima, peke yako kunilea
Hayo yote yamekoma, mkiwa najililia
Machozi kikombe tele (uk.33)

Shairi hili linaonyesha kuwa Amani alikumbwa na huzuni sana kwa kufiwa na wazazi wake hasa mama yake aliyekuwa tegemeo lake baada ya kifo cha baba yake. Katika shairi alilotunga kwa heshima ya mamake, anatamani afe. Kwa hivyo, kifo cha wazazi ni pigo kubwa kwa vijana, kwa sababu ndoto zao za kujiendeleza maishani huzimwa.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, Akida alifiwa na mama yake aliyeangamia katika ajali ya barabarani. Kifo cha mamake Akida kilikuwa pigo kubwa kwake kwa sababu aliishi kwa huzuni kwa miaka mingi. Tunaelezwa kuwa:

> Zaidi ya miaka kumi tangu mama kufa, bado nahisi uchungu moyoni kila nikimkumbukia. Laiti mama angalikuwapo leo, ashiriki furaha na fahari yangu. Nakwenda Tandika kwa mara ya kwanza maishani mwangu. Hilo si dogo. Mama asingaliliona dogo-la mwanawe kwenda kuzuru jiji kuu la nchi yetu Kiwachema...Nakwenda jijini kuzawadiwa na waziri...Mama! Mama! Laiti ungalikuwa hapa utabaruku

> katika furaha na fahari yangu. Mama! Ni hapa Tungule ndipo ulipofia (uk. 1)

Kijana huyu daima anakumbwa na huzuni kila mara anapomkumbuka mama yake. Mbali na kuhuzunika, Akida aliachiwa jukumu la kumtunza baba yake ambaye alikuwa anaugua. Jambo kama hili huwa ni mzigo mzito sana kwa mtoto. Tunaambiwa:

> Mama katuacha mikono miaka kadha iliyopita, baada ya basi alimokuwa akisafiria kugongana na lori. Baba alikuwa naye kavimba miguu, sijui kwa matende au maradhi gani. Dhima ya kumtunza iliniangukia. Haikuhalisi kumwacha baba peke yake na kwenda kujifurahisha nafsi yangu jijini (uk. 10)

## 3.4 Kukatizwa kwa masomo ya vijana

Elimu ndio uti wa mgongo wa mafanikio katika maisha siku hizi. Kwa hivyo, ni jambo la muhimu kwa vijana kupewa elimu ili waweze kujiendeleza maishani na hata kuendeleza jamii kijumla. Hata hivyo, kuna vikwazo ambavyo huwazuia vijana kujiendeleza kimasomo. Baadhi ya mambo ambayo huwafanya vijana kukatiza masomo yao ni kama vile ukosefu wa karo kwa sababu ya umaskini, mimba kwa wasichana wakiwa bado shuleni, mapenzi ya kiholela baina ya vijana, tamaduni zilizopitwa na wakati kama vile ndoa za mapema na tohara, miongoni mwa mengine mengi. Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Kufa Kuzikana*, mwandishi ameonyesha baadhi ya mambo ambayo yamewafanya vijana kutokamilisha masomo yao. Suala la vijana kukatiza masomo yao linakuwa changamoto kubwa kwa sababu wanakosa kufuzu ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Imani anasononeka sana kwa sababu masomo yake yalikatizwa kwa sababu ya umaskini. Mama yake alikuwa na uhaba wa fedha ndiposa akashindwa kumlipia karo yeye na ndugu zake. Imani alikuwa anatamani kusoma hadi chuo kikuu na akihitimu awe daktari awatibu wagonjwa vizuri ili wasife kwa sababu ya mapuuza ya madaktari. Huu ndio mchango wa mabadiliko alinuia kuleta maishani mwake na kwa jamii yake. Ndoto yake haikutimia kwa sababu ya umaskini.Tunaelezwa kuwa:

> Mama alikuwa na uchefuchefu wa fedha akashindwa kutulipia karo. Nilisononeka sana masomo yangu yalipokatizwa nilipokuwa kwenye mpaka kati ya shule ya msingi na shule ya upili. Nilitamani nisome hadi chuo kikuu niwe daktari, niwatibu wenye ndwele kama ndugu yangu mwingine aliyekufa kwa mapuuza ya madaktari. (uk.56)

Mashaka naye ni kijana mwingine ambaye masomo yake yalikatizwa. Mashaka alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Ben Bella Maozi. Mashaka alikuwa bintiye Mtemi Nasaba Bora ambaye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Lowela, dada yake Ben Bella Maozi. Ben Bella alipogundua kuwa baba yake Mashaka alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na dadake Lowela, aliamua kuvunja uhusiano wake na Mashaka. Ben Bella alimwandikia Mashaka barua na kumwambia kuwa baba mkwe hawezi tena kuwa shemeji. Mashaka alipopokea barua hiyo, aliathirika sana na akaamua kuacha shule. Tunaelezwa:

> Tangu Mashaka aipokee barua toka kwa Ben Bella, alikuwa mnuni, kainama kama kondoo... Alikuwa akiugua " Sononi na shida'' za mapenzi ya waachanao. Alianza kuwa na mahoka hata wenzake shuleni wakaanza kumuambaambaa. Barua ya Ben Bella ilikuwa imeiporomoa imani aliyokuwa nayo kwa babake Mtemi Nasaba Bora. Punde tu baada ya kaka yake kuguria Songoa, Mashaka alikatiza masomo yake na kurudi nyumbani. Akaapa kutorudi skulini ima fa ima. Wazazi wake walipojaribu kumwamrisha arejee skulini ilikuwa sawa na kusema na kisiki, hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. (uk. 121)

Masomo ya Mashaka yalikatizwa kwa sababu ya kujihusisha katika mapenzi akiwa anaendelea na masomo yake. Hii ni changamoto kubwa kwa sababu Mashaka ni msichana ambaye angesoma sana na kuleta mabadiliko katika jamii yake vile alitazamia, kwa vile wazazi wake walikuwa na uwezo wa kumsomesha, lakini alikatiza masomo yake kwa sababu ya mapenzi. Mbali na kukatiza masomo yake, Mashaka anakuwa mzigo kwa familia yake alipopatwa na kichaa kwa sababu ya Ben Bella kukatiza mapenzi yao.Tunaelezwa:

> Tangu akatize masomo yake baada ya kusoma barua ya Ben Bella, Mashaka hazimtoshi. Alibwabwaja ovyoovyo kama Mzee Matuko Weye. Mara mbili alitaka kujinyonga akazuiwa. Alizitupa nguo na kuzurura tupu mitaani. Bi Zuhura alimeza mate machungu. Kichaa cha Mashaka kilikuwa kwake kuelekeza msumari moto kwenye donda. Hakujua kilichomharibu akili bintiye mzuri na mwema. (uk. 129)

Masomo ya Amani yalikatika alipokuwa chuo kikuu, mjini Songoa. Watu ambao walimwonea wivu kwa kufaulu masomoni walimtilia fitina mpaka akaacha masomo yake na akafungwa jela.Tunaelezwa:

> Kusema kweli niliwahi kuwa chuo kikuu mjini Songoa.Wapo walionionea gere kwa ufanifu wangu masomoni, wakaniponza. Kila mtihani niliofanya tangu shule ya msingi hadi chuo kikuu niliongoza taifa zima. Basi ingawa sikupenda siasa, wanafunzi hao walificha karatasi za uchochezi chumbani mwangu na kuniitia askari. Askari walifika na kupiga sachi wakazitoa karatasi hizo. Nilifungwa jela miaka mitano. Nikumbukapo nalia machozi ya kuweza kuunga mito. (uk.117)

Amani alikuwa mwanafunzi mwerevu sana. Angemaliza masomo yake ya chuo kikuu angechangia kuleta mabadiliko na maendeleo katika jamii yake. Hii ni kwa sababu mambo ambayo tayari ameyafanya katika jamii yake ni makubwa hata bila kuhitimu masomo yake ya chuo kikuu. Kwa hivyo, kukatiziwa masomo yake kwa sababu ya fitina kunamnyima fursa ya elimu bora.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, Akida naye alikuwa mwanafunzi mwerevu sana shuleni aliyependa masomo yake. Katika mtihani wa taifa wa shule za msingi, Akida alikuwa miongoni mwa watahiniwa watatu bora kote nchini Kiwachema. Alikuwa mmoja wa wale watatu bora waliozawadiwa na Waziri wa Elimu. Alipokuwa akihojiwa wakati wa kuzawadiwa, alisema kuwa alinuia kusoma sana hadi awe msanifu ujenzi na kuzuia ajali zinazosababishwa na majengo yaliyojengwa vibaya kwa sababu ya ufisadi. Alikuwa na ndoto nzuri sana ya kuleta mabadiliko

katika jamii baada ya kuhitimu masomo yake lakini masomo yake yalikatizwa wakati vita vya kikabila vilizuka nchini mwake. Walipopashwa habari za kuzuka kwa vita wakiwa jijini, Akida alishituka sana na kujiuliza maswali kama haya:

> Je, babangu hajambo? Je, nitawahi kumwona tena?...Je, ninao mustakabali wowote? Nitawahi kwenda shule ya kitaifa ya upili ya nafasi? Nitasoma niwe msanifu ujenzi maarufu nchini? Au matamanio yangu yameyeyushwa na kutokomezwa na vita vilivyozuka kwetu kijijini? (uk.65)

Maswali haya yanaonyesha vile Akida alitamaushwa na vita vya kikabila vilivyochipuka kijijini mwao. Vita hivi vya kikabila viliendelea mpaka Akida akakosa kuendelea na masomo yake ya shule ya upili na pia babake mzazi akauawa.

Susana aliachishwa masomo na wazazi wake walioshikilia mila na tamaduni ili aolewe. Baadhi ya tamaduni katika jamii kama tohara hasa ya wasichana na ndoa za mapema huwa zinawafanya vijana wa kike kukatiziwa masomo yao na kutofikia matamanio yao maishani. Mwandishi anasema; "Susana alikuwa kigoli aliyekatiza masomo kwenye darasa la sita ili aonje tamu na chungu ya ndoa." (uk.178)

Jerumani ni kijana ambaye alikuwa akisomea uhandisi katika Chuo Kikuu cha Koln. Akiwa mwaka wa pili, masomo yake yalikatizwa na akarejea nchini Kiwachema kwa sababu ya ubaguzi wa rangi. Kijana huyu angekuwa na mustakabali mzuri sana na angeleta maendeleo katika nchi yake iwapo angekamilisha masomo yake na kuwa mhandisi. Hata hivyo, masomo yake yalikatizwa. Anamwelezea kijana mwenzake Akida vile alivyorejea nchini Kiwachema:

> Nawe nini kilichokurejesha huku? "Usinikumbushe hayo bwana. Wajerumani wameendelea kweli lakini wanamchukia mtu mweusi. Mtu unaonewa tu kwa sababu ya rangi ya ngozi yako, ushafahamu? Nilikuwa nasomea uhandisi katika Chuo Kikuu cha Koln, nimo mwaka wa pili. Nikawaona *skin heads* wanne wanamshambulia mwanamke mweusi burebure akiwa na kitoto chake kidogo nje ya Café Charmonte. Sioni dhuluma nikatulia. Nikawarushia ngumi nzitonzito kama mwendawazimu. Wacha wanigeukie. Walinitwanga mpaka nikaona

> vimulimuli. Nilikamatwa na polisi bwana... Nilifungwa jela miaka saba...Nilipomaliza kula kalenda nikarejeshwa Kiwachema kwa nguvu...Serikali ya Ujerumani iliyokuwa inafadhili masomo yangu ikaondoa ufadhili na ufadhili wenyewe nilikuwa nimepewa kwa kuwa *best student* kwenye kitivo cha uhandisi katika Chuo Kikuu chaTandika. (uk. 155)

### 3.5 Umaskini

Umaskini ni hali ya kutokuwa na mali. Mtu akiwa na ukosefu wa mahitaji ya msingi ya binadamu kama vile chakula, maji, makazi, usalama, huduma za afya na mavazi kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kuvimudu husemekana kuwa ni maskini. Katika jamii nyingi, watu wengi ni maskini wakilinganishwa na matajiri. Kwa hivyo, umaskini umekuwa kikwazo cha maendeleo katika jamii. Tatizo la umaskini lilianza tangu jadi wakati wakoloni walitawala nchi za Kiafrika. Hali hii ya umaskini iliendelea hata baada ya uhuru kwa sababu viongozi waliochukua hatamu za uongozi baada ya mkoloni kuondoka, walikuwa wabinafsi kwa sababu waligawa rasilimali za kitaifa bila usawa. Hali hii imeendelea kutoka kizazi kimoja hadi kingine na huwa inaathiri sana vijana hasa wakati wanapojaribu kupambana na uovu katika jamii na kueleta mabadiliko kwa sababu watakuwa hawana uwezo wowote. Hali hii imedhihirika vema miongoni mwa wahusika ambao wanajaribu kuleta mabadiliko chanya katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Kufa Kuzikana*.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Imani alilelewa katika hali ya umaskini. Imani anamwelezea Amani vile walinyang'anywa kijishamba walichoachiwa na baba yake ambapo mama yao aliuliwa na wao wakabaki bila makao. Jambo hili liliwafanya kuishi hali ya kimaskini kabisa na ndiposa alikuwa ameamua kujitosa majini afe. Imani anasema kuwa mama yake hakuwa na fedha za kutosha kuwalipia karo. Imani anaendelea kuelezea jinsi askari walitumwa kuja kuwapokonya shamba lao. Anasema:

> Ulikuwa wakati wa adhuhuri hivi, walipokuja askari na bastola mikononi wakamwambia mama kuwa wametumwa kumwamrisha ahame haraka iwezekanavyo toka kwa shamba la mwenyewe. Mama akawaambia kuwa yeye ndiye mwenyewe. Akawatolea hatimiliki wakamnyaka makofi na kuondoka. Wakamwonya kuwa wangerudi tena

> naye angejua kilichomfanya sangara kuchomwa moto...Baada ya mwezi mmoja walirudi tena wakasema kwamba wametumwa kumwondoa mama na aila yake katika shamba hilo la mwenyewe...Wakatoa hatimiliki nyingine ya shamba hilo... Kisha wakaondoka tena na kutuacha hapo tukiwa hoi. Mama aliugua na kukata roho kutokana na kipigo alichopigwa. (uk. 56)

Kitendo hiki cha Imani kushuhudia mamake akipigwa kinyama kilimwathiri sana. Anasema kuwa akumbukapo huhisi uchungu mwingi moyoni. Baada ya muda, mamake Imani aliugua na kukata roho kutokana na kipigo alichopigwa. Kifo cha mama huyu kilikuwa pigo kubwa kwao kwa sababu ndiye aliyekuwa tegemeo lao. Oscar aliondoka kwenda kusikojulikana, naye Imani akatoroka baada ya kunusurika kuteketezwa ndani ya nyumba yao. Jambo hili liliwafanya vijana hawa kuendelea kuishi maisha ya kimaskini kwa sababu hawakuwa na pahali pa kuishi.

Taswira ya kijana DJ na wenzake walipokuwa wakioga katika Mto Kiberenge inaonyesha hali ya umaskini uliokithiri. Mwandishi anasema:

> Kivulana chenyewe kifyefye kilichodhoofika sana kiafya. Mwili mwembamba kama sindano. Kiliposimama kama kilivyozaliwa na kujikunakuna mgongoni, ungeweza kuona kwa mbali upele ulivyoihujumu ngozi yake ya maji ya kunde. Nywele nyekundu labda kutokana na utapiamlo. (uk. 6)

DJ alikuwa mchungaji aliyewachunga ng'ombe wa matajiri tofauti wa Sokomoko. Baadaye, anawaelezea Amani na Imani kuhusu maisha yake. Tunaelezwa:

> Bila kutarajiwa, DJ aliwasimulia maisha yake. Alikuwa mtoto wa mjane aliyepika pombe haramu kwenye mtaa wa Madongoporomoka mjini Songoa. (uk.9)

Vijana wakilelewa katika hali ya umaskini kama hii inakuwa ni changamoto kubwa kwa sababu wana nafasi finyu sana ya kuweza kuleta maendeleo katika jamii zao. Umaskini huwakosesha elimu kwa sababu wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia karo. Pia, vijana wakikaa katika mazingira chafu wanaweza kupatwa na maradhi ambayo yatadhuru afya zao kama vile DJ alikuwa na upele.

utumizi wa dawa za kulevya, wizi na ukahaba unaowahatarisha kuambukizwa magonjwa ya zinaa na ukimwi.

### 3.6 Mihadarati na pombe

Mihadarati ni dawa za kulevya. Dawa za kulevya zinaweza kuwa kizuizi cha maendeleo hasa zinapotumiwa na vijana. Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Ben Bella Maozi alikuwa na uraibu wa bangi na ashiki wa muziki wa kufokafoka. Utumiaji wa bangi unamfanya ajiingize katika mapenzi ya kiholela na msichana anayeitwa Mashaka; mapenzi ambayo baadaye yalimfanya Mashaka kuingiwa na kichaa. Ben Bella pia alikuwa sugu wa jela. Alifanya maovu mengi kama ubakaji wa watoto wadogo. Tunaambiwa:

> Ben Bella alikuwa lofa aliyekuwa na uraibu wa bangi na ashiki wa muziki "wa kufokafoka". Alizoea kuvaa suruali yenye upana iliyompwaya na fulana yenye maneno"niguse uone." Alikuwa sugu wa jela. Aliingia jela na kutoka kama nyumbani. Alikuwa katoka jela karibuni baada ya kula kalenda miaka miwili kwa tuhuma ya kukibaka kitoto kidogo. (uk .79)

Maovu kama haya yanatokana na utumiaji wa mihadarati na vijana wakijiingiza katika matendo kama haya huondoa matumaini ya wao kuwa na manufaa katika jamii zao.

Katika *Kufa Kuzikana*, tunaelezewa madhara ya pombe katika jamii. Akida anaeleza alichoshuhudia katika klabu moja ya pombe. Anasema kuwa mwanamke mmoja mwenye jirimu la kiboko alimwendea na kumuuliza alitaka pombe baridi au moto, lakini yeye alijibu kwa kutikisa kichwa tu. Maneno aliyoyasikia Akida yakizungumzwa na walevi ni ya kutia shaka kwa vile walikuwa wakijigamba vile walikuwa wamewaua Wakanju:

> Nakwambia tuliwafyeka Wakanju. Korosho hawawezi kurudi tena... Mwenyewe usinione hivi nimeua Wakanju wengi sana. Usione wembamba wa reli, garimoshi hupitia. (uk. 132)

Tangu Jerumani akatize masomo yake huko Ujerumani, alikuwa akivuta bangi, sigara na kulewa pombe ili kujipoza. Akida anaelezea aliyoyaona alipomtembelea:

> Alinitungia macho na kutikisa kichwa. Waniona hambe sio? Au unafikiri bangi imenizidi? Njoo kwangu leo jioni nikuonyeshe...Ukutani kulikuwa na picha kuukuu ya mbunge wetu Johnstone Mabende, macho yametobolewa mashimo. Aidha harufu ya sigara ilichanganyika na ile ya pombe aina ya gongo tokeo likawa mseto wa kukirihisha (uk.157)

Tatizo la dawa za kulevya limekuwa janga kubwa duniani kote. Watu wengi hasa vijana wameathirika na janga hili. Vijana wengi wamejiingiza katika janga la kutumia, kuuza na kusafirisha dawa za kulevya. Dawa hizi ni hatari kwa mtumiaji kwa sababu huweza kuvuruga akili na kufanya mtu afanye mambo ya kinyama. Kwa mfano, ubakaji, ujambazi na kuua kati ya mengine.

### 3.7 Mapenzi ya kiholela

Siku hizi vijana wengi hujihusisha katika mapenzi na ngono kabla ya ndoa, na kuliona kama jambo la kawaida. Kwa kufanya hivi vijana hupoteza mwelekeo kwa kuishi kiholela bila ya kuwa na mwongozo mwema katika maisha yenye mafanikio sasa na baadaye. Uwezo na fursa ya vijana ya kuishi maisha bora hupotea, kwa sababu ya athari zinazotokana na mapenzi ya kiholela. Kwa mfano, mapenzi na ngono za kiholela huzaa wivu, tuhuma mbaya na majanga ya kijamii. Wasichana wanaoanza ngono kabla ya ndoa wanaweza kuwa na maisha magumu ya baadaye kutokana na kuacha masomo au kuzaa ovyoovyo bila mpangilio. Baada ya tendo hili, huenda mvulana akamwona msichana havutii tena kimahaba na kumchukia sana. Hili linaweza kumfanya msichana kupata athari za kisaikolojia na hata akarukwa na akili.

Mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea* ameangazia vijana ambao walijiingiza katika mapenzi ya kiholela na matokeo yake. Mfano mojawapo ni Fao ambaye alimtunga mimba msichana wa shule. Fao alikuwa amekamilisha kidato cha nne alipopata ajira ya muda kama mwalimu asiyehitimu wa shule ya sekondari ya Ulitima, akingojea kwenda chuo kikuu. Alishindwa kujizuia kumpenda msichana mmoja mwanafunzi. Msichana mwenyewe naye hakukataa na akakubali kujihusisha katika mapenzi ya kiholela na mwalimu wake. Msichana huyu alipojifungua, wazazi wake waliamua kumpelekea Fao mtoto wakiwa wamekasirika sana na

kudai kuwa Fao aliwaharibia binti yao kwa kumringa. Fao alipowaona alitorokea dirishani na kuwaachia wazazi wake na dadake mzigo wa kumlea huyo mtoto. Tunaelezwa hivi:

> Matokeo yalipotangazwa wote walikuwa wameupita mtihani...Wakiwa wote wanasubiri kwenda chuo kikuu, wakapata ajira ya muda kama walimu wasiohitimu wa shule ya sekondari ya Kinondani kwao Ulitima. Hapo ndipo Fao alipojigeuza paka kulinda kitoweo. Akashindwa kujizuia kumpenda msichana mmoja mwanafunzi. Hakujidhibiti kama impasavyo kila mwalimu bora. Naye binti ya watu mwenyewe katarajia kukanyaga miiba bila viatu na kutegemea hatadungwa hata mwiba mmoja. (uk.36)

Walipokuwa wakiendelea na mazungumzo, mtoto huyo aliingia barazani, ndipo dadake Fao akaanza kumwelezea Amani jinsi wazazi wa msichana huyo mwanafunzi ambaye Fao alimpenda walivyomletea Fao mtoto huyo kwa fujo. Kitendo kama hiki kinaweza kusababisha uhasama kati ya vijana na hata wazazi wao na kuwa kizuizi cha maendeleo. Vijana wakijiingiza katika mapenzi ya kiholela watapatwa na maafa, wasiweze kutulia na kujenga maisha yao ya baadaye. Kwa mfano, ilimbidi Fao atoroke na kuacha kazi yake ya ualimu alipowaona wazazi wa msichana aliyemtunga mimba wakimletea mtoto. Msichana aliyetungwa mimba naye aliacha masomo yake ili akajifungue.

Dadake Fao naye alikuwa amewahi kujihusisha katika mapenzi na akazaa mtoto kabla ya kuolewa. Vijana wakipata watoto kabla ya kuolewa ni changamoto kwao kwa sababu ya malezi watakayowapa watoto hao. Hii ni kwa sababu malezi ni mchakato changamano ambao unajumuisha mambo mengi yakiwemo lishe bora, mavazi, makao, elimu, pamoja na ushauri mwafaka. Kwa hivyo, wazazi wote wawili wanahitajika ili kusaidiana kumlea mtoto.Vinginevyo, kijana atakayeachiwa malezi akiwa peke yake atalemewa bila shaka.

Lowela ni msichana ambaye alijihusisha katika mapenzi na ngono kiholela na Mtemi Nasaba Bora. Alipogundua kuwa amepata mimba, aliificha na kujifungua kisiri. Baada ya kujifungua walifanya njama na Mtemi Nasaba Bora ili wampeleke mtoto kwa kibanda cha Amani aliyekuwa akichunga mifugo kwa Mtemi Nasaba Bora. Usikuusiku Mtemi Nasaba Bora alikibeba kitoto

hicho na kukiacha mlangoni mwa kibanda cha mchunga wake ili kionekane kama ni chake. Mtemi alifanya hivi kumzuia bibi yake asitambue kuwa alikuwa na jicho la nje na pia Lowela asijulikane na wazazi wake kuwa alikuwa amezaa kabla ya ndoa. Tunaelezewa jinsi Bi. Zuhura alivyoshangaa. Amani alimpelekea hicho kitoto baada ya kukiokota mlangoni mwa kibanda chake.

Kitendo kama hiki ni cha kuatua moyo kwa Amani kwa sababu tayari alikuwa amelemewa na maisha. Kwa hivyo, kumuongezea mzigo wa kulea mtoto ni changamoto kubwa kwake. Mwajiri wake Mtemi Nasaba Bora alimtaka Amani aendelee na kazi kama kawaida licha ya kuwa alikuwa na mtoto mdogo kama tunavyoelezwa; "Amani akakitwaa kile kitoto kichanga na kutoka nacho. Alipofika mlangoni, alisikia sauti ya Mtemi ikitoa amrisho; usisahau kukama ng`ombe na kuwapeleka malishoni."(uk.42)

Mashaka ambaye ni bintiye Mtemi Nasaba Bora alijihusisha katika mapenzi na Ben Bella. Baadaye, Ben Bella aliamua kuyakatiza mapenzi yao jambo ambalo lilisababisha Mashaka kukatiza masomo yake na mwishowe akapatwa na kichaa kwa sababu hakuamini penzi lake kwa Ben Bella lingekoma.Tunaelezewa hivi:

> Tangu Mashaka aipokee barua toka kwa Ben Bella, alikuwa mnuni kainama kama kondoo... Alikuwa akiugua "sononi na shida'' za mapenzi ya waachanao.... Mashaka alikatiza masomo yake na kurudi nyumbani. Akaapa kutorudi skulini ima fa ima...Tangu akatize masomo yake baada ya kusoma barua ya Ben Bella, Mashaka hazimtoshi. Alibwabwaja ovyoovyo kama Mzee Matuko Weye. Mara mbili alitaka kujinyonga akazuiwa. Alizitupa nguo na kuzurura tupu mitaani. Bi Zuhura alimeza mate machungu. Kichaa cha Mashaka kilikuwa kwake kuelekeza msumari moto kwenye donda. (uk.129)

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, Akida alijihusisha kimapenzi na msichana aliyeitwa Susana, jambo ambalo linamfanya Susana kuacha masomo yake na kuolewa. Akida anaelezea vile mambo yalivyoanza:

> Nilimdondokea msichana mmoja rafiki ya Cynthia, jina lake Susana. Walikuwa wakisoma pamoja na kutembeleana sana. Mambo yalianza kwa kukonyezeana macho hadi tukajikuta tumetumbukia katika lindi la mapenzi na makosa mazito; dhambi hasa. Kila baada ya 'tendo' nikihisi hatia hususan nilipokumbukia mahubiri ya kasisi John Njalala jijini Tandika. Nilishangaa mno Susana alipokatiza masomo na kuolewa na Joseph.(uk.169)

Mapenzi ya kiholela huchangia vijana wa kike kupata mimba zisizotarajiwa. Wasichana hawa huishia kupata watoto na kuwalea bila kusaidiwa na wanaume waliowatunga mimba kwa sababu mara nyingi wanaume hawa huwahepa baada ya kugundua kuwa wamehimili. Jambo hili hukosesha ulezi mzuri kwa sababu watoto wanaozaliwa hukosa mapenzi na mahitaji ya kimsingi kutoka kwa wazazi wote wawili. Wasichana wakipata ujauzito wakiwa shuleni hukatiza masomo yao na jambo hili huathiri maisha yao ya siku za usoni kwa sababu bila elimu hawataweza kupata kazi nzuri itakayowawezesha kuyamudu mahitaji yao.

### 3.8 Mila na imani zilizopitwa na wakati

Jamii nyingi za Kiafrika zilikuwa na tamaduni na imani ambazo zilifuatwa na kila mwanajamii ili kuhakikisha kuwa watu waliishi kwa umoja na utangamano. Hata hivyo, baadhi ya tamaduni na imani hizo zimegunduliwa kuwa na madhara hasa katika karne hii ya ishirini na moja ambapo watu wameelimika. Kupitia kwa fasihi ambayo huchukuliwa kuwa kioo cha jamii, baadhi ya tamaduni ambazo zinaonekana kuwa zimepitwa na wakati zimeangaziwa. Tamaduni hizi zinaweza kuwa kisiki na kuzuia wanajamii wasipate kuendelea. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* mwandishi ameangazia tamaduni ambazo zimekuwa changamoto kwa vijana wanaotaka kuleta maendeleo katika jamii. Tim na Janelle wanapozungumziana wanataja baadhi ya mila katika jamii yao na kuziona kama zilizopitwa na wakati na kupendekeza kuwa zinapaswa kutupiliwa mbali kwa sababu zinarudisha nyuma maendeleo. Tunasoma hivi; "Baadhi ya mila zimepitwa na wakati; bora zitupwe kwenye kapu la sahau," alisema Tim.(uk.83)

Wakati babake Tom aliaga dunia, kulikuwa na ubishi kuhusu mahali atakapozikwa. Tom alikuwa anataka babake azikwe huko kijijini kwao Baraki kulingana na mila. Wakati huo vita vya

kikabila vilikuwa bado vinaendelea na ndiposa Tim alimsihi Tom amzike babake kwenye makaburi ya umma jijini. Tim anasema kuwa kwenda kijijini wakati wa vita ni hatari kwa usalama wao na kuwa hakuna haja ya kugharamika bure kusafirisha maiti nyumbani. Tim anamwambia Tom; "Desturi hizo zimepitwa na wakati Tom." (uk.91)

Mila hii ni changamoto kwa sababu inagharimu pesa nyingi sana na hata kuhatarisha maisha yao. Tim alitumia pesa nyingi sana kulipa askari ili wamsindikishe hadi Baraki kwa shughuli za mazishi na pia kukodi marafiki watakaomsaidia kuchimba kaburi. Tim alikuwa karibu kupoteza maisha yake baada ya kuvamiwa walipokuwa wakiendeleza shughuli za mazishi.

Mila nyingine ambayo inakuwa changamoto kwa vijana wanapotaka kujiendeleza ni tohara ya wasichana. Tohara ya wasichana imeleta madhara mengi na hata kusababisha vifo. Hii ndiyo sababu Jerumani anasema kuwa nchi yao inahitaji mapinduzi; sio mapinduzi ya serikali bali mapinduzi ya ada na mila. Jerumani anamweleza Akida haya:

> Hii nchi yetu inahitaji mapinduzi. Sio mapinduzi ya Serikali, mapinduzi ya ada na mila. Mapinduzi ya mitazamo, misimamo na mikabala. Sisi Wanakiwachema tumelemaa vibayavibaya. Subiri msimu wa tohara ufike uone maajabu. Utawaona wasichana maskini wanalazimishwa kutahiriwa burebure. Wengine watapatwa na blutung mpaka wafe. Mwaka jana wamekufa wawili. Lo! Mila gani hizo za upuuzi? Ndio maana tunabaki nyuma. (uk.154-155)

Mbali na kusababisha vifo, tohara ya wasichana huathiri masomo yao. Haya hutokea wakati ambapo baadhi ya wasichana huamua kutoroka tohara ya lazima. Bi. Tina, mamake Cynthia alifanya mpango na Akida ili amtoroshe Cynthia usiku hadi mjini Sangura kwenye kituo cha wasichana wanaokimbia tohara ya lazima. Wakati huu Cynthia alikuwa bado shuleni. Kwa hivyo, ilimbidi akatize masomo yake. Hii ni changamoto kubwa kwa vijana kwa sababu wanahitaji masomo ili kujiendeleza. Katika harakati za kutoroka, wasichana wanaweza kushambuliwa na wahuni kwa sababu huwa wanatoroka usiku. Akida anaeleza matatizo waliyokumbana nayo njiani; "Sikuwa mweledi wa kuendesha baiskeli wala baiskeli yenyewe haikuwa na kurunzi. Nilimwangusha Cynthia mara tatu hivi. Ulikuwa mwendo wa zapata kilomita arobaine hivi." (uk.170)

Mbali na tohara ya wasichana, tohara ya wavulana pia inasababisha vifo kwa sababu ya kufanywa kwa kutumia njia za kitamaduni na kutekelezwa na ngariba ambaye hana ujuzi. Cynthia anamweleza Akida jinsi alivyoshuhudia tohara ikifanywa na maafa yaliyompata mvulana mmoja:

> Msimu wa ukeketaji wa kisu cha ngariba ukaja. Asubuhi moja nilishuhudia ngariba mmoja chongo akimtahirisha mvulana mmoja karibu na kituo cha biashara cha Binge. Alimkata mpini ukaanguka. Umati ukaanza kumpiga kitutu ngariba. Ni baadaye tu ndipo kijana majeruhi alipopelekwa hospitalini Sangura mjini.(uk.172)

Njia hizi za kitamaduni za kupasha vijana tohara huhatarisha maisha yao na kuwarudisha nyuma kimaendeleo. Kwa hivyo, jamii inapaswa kutupilia mbali tamaduni hizi na kuzingatia njia za kisasa za kutahirisha wavulana kwa sababu wakilemewa huko jandoni, mwishowe ngariba huwapeleka wavulana hawa hospitalini ili watibiwe.

Ndoa za mapema na za lazima ni utamaduni mwingine ambao ni changamoto hususan kwa wasichana. Katika jamii nyingi za Kiafrika, elimu kwa wasichana haikuthaminiwa. Katika karne ya ishirini na moja ambapo elimu kwa vijana imekuwa ya lazima, bado kuna wanajamii ambao hawathamini elimu ya wasichana na kushikilia kuwa wasichana wanapaswa kuolewa wakiwa wachanga. Jambo hili linakuwa changamoto kwa wasichana kwa sababu ya kutojua kusoma na kuandika. Akida alishangaa rafiki yake aliyeitwa Susana alipokatiza masomo na kuolewa na Joseph. Jambo hili lilimfanya Susana kuishi maisha duni na hata kumfanya afedheheke kwa vile hangeweza kusoma hata barua. Tunaelezwa jinsi Bi. Tina alivyoenda kumwita Susana awasomee barua lakini akashindwa. Akida anasema:

> Akaenda kwa Joseph mwana wa mjane na aliyekuwa mumewe Susana na rafiki yangu wa awali. Susana alikuwa kigoli aliyekatiza masomo kwenye darasa la tisa ili aonje tamu na chungu ya ndoa. Susana alikuwa mke mchanga, mbichi na mchafuchafu. Alipopewa barua kusoma alianza kutetemeka na kupenga kamasi ovyoovyo. Alinitupia jicho mara moja kwa haya. (uk.178)

Susana angekuwa amesoma, aibu kama hii aingempata. Changamoto hii imekuwa ikiangaziwa sana katika vyombo vya habari kwa sababu katika jamii, wasichana wadogo wamekuwa wakiachishwa shule na kuozwa bila hiari yao.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, wakazi wa Sokomoko walikuwa hawayanywi maji ya Mto Kiberenge kwa sababu ilikuwa ni mwiko kwao kuyanywa. Waliamini kuwa mwanamume mmoja mgonjwa wa kifafa alifia mtoni humo na maiti yake haikupatikana. Walikuwa hata wametunga wimbo uliotangaza mwiko huu:

Nijapolewa tembo
Nikalewa chakari
Nipepesuke
Nijapovuta kasumba na kuyumba
Niyumbeyumbe
Nikapayuke
Sinywi maji ya Kiberenge
Siyanywi katu siyanywi (uk.4)

Wimbo huu unaonyesha jinsi mwiko huu ulivyokuwa umekita mizizi miongoni mwa wanajamii. Mwiko huu ni changamoto kwa wanajamii, wakiwemo vijana wawili; Imani na Amani waliokuwa safarini kwa sababu hawangeweza kuyanywa maji haya ili kukata kiu. Kiu ilipowakaba sana, Imani na Amani waliamua kuuvunja mwiko huo na kuyanywa maji ya Mto Kiberenge, jambo ambalo liliwashangaza wale walioshuhudia. Hata hivyo, hakuna chochote kilichowatendekea kwa sababu hii ilikuwa imani tu ya jamii isiyokuwa na msingi. Imani kama hizi zinapaswa kutupiliwa mbali kwa sababu huwa zinazuia na kurudisha nyuma maendeleo katika jamii.

### 3.9 Ukosefu wa sera madhubuti za kuwatuza wanamichezo

Vijana wengi huwa wanajishirikisha katika michezo na kuiletea nchi yao sifa si haba wanapofaulu. Hii ni njia mojawapo ambayo vijana wanaweza kuitumia kuiletea nchi yao umaarufu na kuifanya ijulikane duniani kote. Hata hivyo, kunakuwa na changamoto pale ambapo vijana wanaumia wakichezea nchi zao na wakapuuzwa na serikali na kukosa kufidiwa. Kijana aitwaye Chwechwe Makweche alikuwa mwanasoka hodari aliyekuwa akiichezea nchi yake

katika Songoa FC. Kijana huyu alivunjika mguu katika mashindano ya kitaifa, kama tunavyofahamishwa:

> Habari zenyewe zilizomtuturisha moyo Imani zilikuwa kwamba Chwechwe Makweche alikuwa kavunjwa fupaja la mguu wake wa kushoto katika pambano la soka la kimataifa. Bi. Dora ambaye tangu hapo hakuwa na habari kuhusu uhusiano baina ya Imani na Chwechwe Makweche, yule mwanasoka maarufu wa Tomoko aliemewa na kuduwaa. (uk.136)

Baada ya kijana huyu kuumia akichezea taifa lake, hakuna mtu hata mmoja serikalini ambaye alishughulikia matibabu yake. Makweche aliendа kuishi katika eneo la kikabwela ambapo mguu wake ulioza mpaka ukawa kwenye hatari ya kukatwa. Tunaelezewa kuwa:

> Imani alikuwa ameepukana miaka nenda miaka rudi na kakake mpendwa. Habari za Chwechwe Makweche nduguye kifungua mimba hazikusikika sana tena kwa miezi kadha baada ya tangazo la kuvunjwa fupaja, mpaka mwandishi mmoja wa magazeti mwenye huruma alipomtembelea mwanasoka huyo katika eneo la kikabwela alimoishi jijini Songoa. Mguu uliokuwa unaozeana wenyewe kwa wenyewe ulikuwa katika hatari ya kukatwa ili kuepusha maambukizo. Tokeo la ziara hiyo likawa makala gazetini yenye kichwa; "NIMEKUWA GANDA LA MUA-ASEMA MWANASOKA HODARI." Waswahili husema kwamba "baada ya dhiki faraja," lakini Imani alipomwazia nduguye aliiona ingekuwa sahihi zaidi kubirua mambo na kusema "baada ya faraja dhiki. (uk. 151)

### 3.10 Ukosefu wa umoja na ari ya kuleta mabadiliko

Wakati mwingi, vijana wanapotaka kuibadilisha jamii na kuleta maendeleo huwa wanakumbwa na changamoto pale ambapo wananchi na hata vijana wenzao ambao wangekuwa wanamapinduzi wanafumbwa macho na viongozi ili wasiweze kuona haja ya mabadiliko. Haya yanajitokeza wazi wakati vijana wawili; Madhubuti na Amani wanapojadiliana vile wanaweza kuondoa viongozi wabaya na kuleta mabadiliko katika jamii yao. Tunaelezwa hivi:

> Lakini bila matumaini hatuwezi kwenda mbele na *Revolution.* Kweli kabisa. Lakini historia vilevile imeonyesha kwamba kila mara baada ya mapinduzi, matumaini huzidi uhalisia na matokeo yakawa hasa ni kubadili hali mbaya moja kwa hali nyingine mbaya zaidi na viongozi madhalimu kwa madhalimu zaidi. Aidha, kuna masuala ya wanamapinduzi kufumbwa macho na mihemko, na vizazi, na jeuri, na hasira matokeo yakawa maafa juu ya maafa. Ukiwa navyo vitu hivi kuwaelekea watu wengine ni sawa na kunywa sumu wewe mwenyewe na kuwategemea wao wafe. (uk. 119)

### 3.11 Chuki na fitina

Chuki ni tabia ya kutopenda watu na kutumia maneno ya kugombanisha watu au kufitini. Tendo hili la kuchongea mtu au kumfitini kwa mambo ambayo hajafanya linaweza kusababisha maafa mabaya kwake na kumrudisha nyuma kimaendeleo. Vijana wakifitiniwa wanaweza kupoteza muda wao na nafasi muhimu, ambao wangetumia kujiendeleza na kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao. Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Amani ni mfano mzuri wa wale ambao wamewahi kufitiniwa kwa sababu ya chuki na maisha yao kubadilika. Alipokuwa chuo kikuu mjini Songoa akiwa mwaka wa pili, wanafunzi waliomwonea wivu walimsingizia kuwa ndiye aliyezua uchochezi chuoni. Walificha karatasi za uchochezi chumbani mwake na kumwitia askari.

Amani alikamatwa na kufungwa jela miaka mitano ambapo masomo yake yaliishia kukatizwa. Isingekuwa uchochezi huu, Amani angekamilisha masomo yake, akawa mtu mashuhuri ambaye angeiongoza nchi yake vizuri na kuleta mabadiliko katika nchi. Hii ni kwa sababu hata bila kukamilisha hiyo elimu ya chuo kikuu, alikuwa na maono mazuri kuhusu uongozi. Hii ndio sababu baada ya kifo cha Mtemi Nasaba Bora, wananchi walikuwa wanapendekeza Amani awe mtemi mpya. Amani anakumbuka kifungo hicho kwa uchungu mwingi akisema kuwa hata kilimkosesha kuhudhuria mazishi ya mamake mzazi. Tunaelezwa:

> Wanafunzi hao walificha karatasi za uchochezi chumbani mwangu na kuniitia askari. Askari walifika na kupiga sachi wakazitoa karatasi hizo. Nilifungwa jela miaka mitano. Nikumbukapo nalia machozi ya kuweza kuunga mito. Kufungwa kulikonikosesha maziko ya mamangu mzazi aliyekuwa kajisabilia

> kwangu. Bila mama nisingekuwa mtu achia mbali kuwepo. (uk.117)

Amani alisingiziwa tena na Mtemi Nasaba Bora, wakati Mtemi alijihusisha kimapenzi na Lowela na wakapata mtoto Uhuru. Mtemi aliamua kukileta kitoto hicho kwa kibanda cha Amani na kumsingizia kuwa ndiye babake. Kitendo hiki kilichangia Amani kufungwa jela wakati mtoto huyu alipokufa kwa kusingiziwa tena kuwa ndiye aliyemuua akiwa na mwenzake Imani. Tunaelezwa kuwa:

> Alfajiri kuu Amani alikuwa katika lepe zito la usingizi. Mavune ya kutwa yaliyotangulia yalimwacha yu hoi, katambarika si kidogo. Usingizi ulimparamia kwa nguvu akalala fo fo fo wala hakujipindua kwenye kitanda chake cha teremka tukaze mpaka alfajiri. Alikuwa akisona misono mikubwa alipozindushwa ghafla na sauti ya kitoto kichanga. Akatega sikio kwa makini. Kitoto hicho kiliendelea kulia ng'aa! ng'aa! Akalirusha kando blanketi lake kuukuu na kunyanyuka. Kilio cha kitoto kile bila shaka kilitokea pale nje karibu na mlango. Aliingiwa na mtapo. Akapapasapapasa na kuitwaa kaptura yake ya kaki. Akaivaa marshimarshi na kuufungua mlango uliokomolewa kwa msumari mrefu uliopindwa. Alipoutoa mguu wake wa kwanza nje, nusura akikanyage kitoto kilichokuwa kinapiga usiahi mkubwa. Kilikuwa kitoto kichanga ambacho hakijamaliza hata siku moja tangu kuzaliwa. (uk.34)

Amani alipoletewa kitoto hiki, hakuwa na budi kukilea kwa sababu Mtemi Nasaba Bora Alishikilia kuwa ni chake. Aliamua kuomba usaidizi wa dadake Imani ili wapate kukilea pamoja. Baada ya muda, kitoto hiki kilipatwa na ugonjwa na kikafa. Mtemi Nasaba Bora aliwasingizia Amani na Imani kuwa ndio walikiua na kuamrisha wafungwe gerezani. Tunaambiwa kuwa:

> Askari wa Mtemi walijihimu mapema kuja kuwatia mbaroni Amani na Imani kwa tuhuma za uuaji wa kitoto kichanga, Uhuru. (uk.83)

Wakati mmoja Mtemi Nasaba Bora alipokuwa ameenda kwa shughuli zake usiku, mkewe Bi. Zuhura alimwita Amani chumbani mwake amsaidie kumwua nyoka ambaye alikuwa ameingia

mvunguni. Walipokuwa wakijaribu kumtafuta nyoka huyo, Mtemi Nasaba Bora alirudi. Mtemi alipoingia chumbani mwake na kuwapata Bi. Zuhura na Amani, alimsingizia Amani kuwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na bibi yake. Aliamua kumtandika Amani kwa bunduki mpaka akawa mahututi. Tunaelezewa kuwa:

> Mtemi Nasaba Bora alisimama kwa kitambo kirefu akitia na kutoa la kufanya. Bi. Zuhura na Amani walisimama tu wima, nyoyo zinawadunda. Baada ya Mtemi Nasaba Bora kujiuliza na kujijibu mwenyewe akaenda kwenye sefu yake akaifungua na kutoa bunduki ya mrao. Akaja juu kama moto wa kifuu. Akafoka na kutukana, na akutukanaye hachagui tusi. Akashika mdomoni mwa bunduki hiyo na kumpiga Amani kwa liwato kichwani kwa nguvu zake zote. Amani akabwagika sakafuni kama gunia la mboga...Kwa siku nyingi Amani hakujijua hakujitambua. Alipata fahamu adhuhuri moja yenye joto kali. Alikuwa kalazwa kitandani. Kilichomzindua ni halambe halumbe za muuguzi mmoja wa kike aliyekuwa anabadilisha shuka katika kitanda hicho. (uk.132)

### 3.12 Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili changamoto zinazowakumba vijana katika harakati za kuleta mabadiliko katika jamii. Ni wazi kwamba mwandishi wa *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea* ameyashughulikia masuala ambayo yanaweza kuwakumba vijana wakati ambapo wanajaribu kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao. Masuala yaliyojitokeza ni kama vile; ulemavu, uyatima, kukatiza masomo, umaskini, mihadarati, mapenzi ya kiholela, kusingiziwa, kutoshughulikiwa na wanamapinduzi kufumbwa macho.

Uhalisia wa uyakinifu wa kijamii unajitokeza kwa sababu vijana kama mojawapo wa wanajamii wamejaribu kuyatatua matatizo katika jamii zao ambayo huwa ni kikwazo katika jamii inapotaka kujiendeleza. Hata hivyo, kuna changamoto nyingi ambazo vijana hukumbana nazo katika harakati za kutaka kuleta mabadiliko.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, muhtasari wa sura zilizotangulia za kazi hii umetolewa. Sura hii imeshughulikia matokeo ya utafiti wetu kwa mujibu wa malengo tuliyodhamiria kuyafikia. Pia baadhi ya matatizo ambayo tulikumbana nayo katika kutafiti kazi hii yameangaziwa. Pamoja na hayo, mapendekezo ambayo yanaweza kuwafaa watafiti wa baadaye katika mada kama hii yametolewa.

## 4.2 Muhtasari wa matokeo

Katika utafiti huu, tumechunguza mchango wa vijana katika jamii. Pia tumeshughulikia baadhi ya changamoto ambazo vijana hawa huwa wanakumbana nazo katika harakati zao za kuleta mabadiliko.Tumeongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Tumeyafikia malengo yetu kwa kusoma riwaya zote mbili za *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea* kwa undani ili tuweze kuwatambua wahusika vijana na kuangalia jinsi kila mmoja ametoa mchango wake katika kuleta mabadiliko na kubainisha changamoto za kila mmoja. Pia tumerejelea kazi za waandishi wengine na pia wataalam wa fasihi ndiposa tukaibuka na kazi hii.

Kazi hii imegawanywa katika sura nne. Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia vipengele vya kimsingi katika tasnifu. Hivi ni pamoja na kuonyesha jinsi suala la utafiti lilichipuka, kutaja malengo ya utafiti, kuelezea nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu, yaliyoandikwa kuhusu mada husika na kuonyesha mbinu za utafiti tulizotumia.

Katika sura ya pili, mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika *Kufa Kuzikana* na *Kidagaa Kimemwozea* umeonyeshwa. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, vijana waliojadiliwa ni akina Akida, Tim, Cynthia, Tom, Jerumani, Pam, Tamari na vijana wa chuoni Tandika. Mifano ya vijana hawa katika *Kidagaa Kimemwozea* ni kama vile Amani, Madhubuti, Imani, mrembo kwenye matwana, Lowela, Bob DJ, Mashaka na vijana wa Chuo cha Mkokotoni (Wangwani).

Katika sura hii vijana wamesawiriwa kama mawakala wa mabadiliko. Kwa hivyo, wakipewa nafasi wanaweza kuibadili jamii na kufanya ulimwengu mahali pazuri pa kuishi. Vijana wamejaribu kubadilisha utawala wa nchi kwa kupambana na viongozi wafisadi na wadhalimu. Pia, wamejitolea kuondoa ukabila ambao ni adui mkubwa wa maendeleo ya nchi. Mambo mengine ambayo vijana wameyatilia maanani ni kubadilisha mitazamo ya wanajamii kuhusu masuala kama vile mitazamo kuhusu tamaduni, walemavu, wanyonge, haki za watoto, kisasi na msamaha kati ya mengine.

Sura ya tatu imeshughulikia changamoto ambazo vijana huwa wanapitia wakati wanajaribu kuleta mabadiliko katika jamii. Kubadilisha mambo yaliyozoeleka na watu huwa si lele mama. Kwa hivyo, ni lazima anayetaka kuyabadili akumbane na changamoto si haba.

Changamoto ambazo tumeziangazia katika *Kidagaa Kimemwozea* na *Kufa Kuzikana* ni pamoja na ulemavu, uyatima, kukatiza masomo, umaskini, mihadarati na pombe, mapenzi ya kiholela, chuki na fitina, tamaduni zilizopitwa na wakati, ukosefu wa sera madhubuti ya kuwatuza wanamichezo na ukosefu wa umoja na ari ya kuleta mabadiliko. Vijana wanaonekana kutatizwa na mambo haya, katika bidii zao za kubadilisha jamii. Tumegundua kuwa baadhi ya changamoto husababishwa na vijana wenyewe na nyingine husababishwa na wanajamii ambao huingiliana nao.

Sura ya nne ni hitimisho la utafiti wetu. Tumetoa muhtasari wa kazi yetu na hatimaye tukatoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

### 4.3 Hitimisho

Utafiti huu ulinuia kuonyesha michango ya vijana katika kuleta mabadiliko katika riwaya teule za Kiswahili, kwa kutumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii. Nadharia hii huhusiana na utetezi wa wanyonge na ukombozi wao katika jamii. Katika jamii, kunatokea migogoro kwa sababu kunakuwako na tabaka la wanyonge na tabaka la matajiri. Migogoro hii ndiyo husababisha mapinduzi ya kuwaokoa wanyonge.Vijana wengi waliojihusisha katika kuibadili jamii wanatoka katika tabaka la wanyonge wanaonyanyaswa na matajiri na ndiposa wameinuka na kujitetea huku wakitetea jamii yao kijumla.

Katika kazi hii, imegunduliwa kuwa mitazamo hasi kuhusu vijana hunuia kudhibiti uwezo wao, kwa kuwaona kama duni na wasiokomaa kiakili. Wanajamii walio na mtazamo hasi kuhusu vijana huwaona vijana kama waasi wa maadili ya jamii. Kuna wale wanaowaona vijana kama viongozi wa kesho na kukosa kuwapatia nafasi za kutoa mchango wao katika uongozi. Huu ni mtazamo ambao umepitwa na wakati kwa sababu ulikuwa unatumiwa ili kuandaa vijana kuchukua uongozi baada ya wazee kustaafu, lakini vijana sasa wanashiriki katika uongozi kama vile wazee. Wanajamii wanapaswa kutambua kwamba vijana hupenda kupewa uhuru wa kuishi kwa tafakari zao wenyewe. Maisha hubadilika vile wakati hubadilika na vijana hawana budi kufumbata utamaduni wa kimseto, yaani ule asilia na tamaduni nyingine wanazopokea kupitia elimu. Hata hivyo, kuna mitazamo chanya ambayo husimamia maoni ya wanajamii wanaothamini uwezo wa vijana na kuwaona kama watu wanaoweza kuboresha jamii zao.Vijana ni kiungo muhimu katika kuleta maendeleo, amani na demokrasia. Siku hizi vijana wanashiriki katika kuifunza jamii maarifa na ujuzi mpya kwa sababu kuna mabadiliko mengi ambayo yamejiri hasa ya kisayansi na teknolojia ambayo vijana wana ujuzi mwingi kuyahusu.

Kazi yoyote ile ya utafiti huwa inakumbwa na matatizo ya aina mbalimbali. Katika utafiti wetu, tulikabiliwa na tatizo kuu lililotokana na hali ya utata, ya kuelezea dhana ya kijana. Dhana ya kijana huwa inatolewa vijelezi tofautitofauti kutegemea mambo mbalimbali na pia wataalam tofauti. Hata hivyo, tatizo hili liliweza kudhibitiwa kwa sababu mwandishi wa riwaya teule amebainisha umri wa baadhi ya vijana waliojitokeza katika riwaya zake. Kwa maoni yetu basi, tatizo hili halikuathiri sana uelewa wa tasnifu hii. Tatizo jingine ni uhaba wa vitabu vya marejeleo. Hata hivyo, tulijitahidi ili kupata marejeleo mwafaka yanayohusiana na utafiti wetu.

## 4.4 Mapendekezo

Kwa sababu kazi ya mwandishi mmoja inaweza kuchambuliwa kwa njia tofauti, kazi hii inaweza kuchunguzwa na wahakiki wa siku za baadaye. Hii ni kwa sababu sisi tumejikita tu kwa masuala ya vijana na michango yao katika kuleta mabadiliko. Kwa hivyo, watafiti wa baadaye wanaweza kutafiti mambo mengine kama vile:

1. Mchango wa wahusika wengine kama wazee katika kuibadilisha jamii.
2. Usawiri wa wahusika na jinsi uteuzi wao unavyochangia kuendeleza dhamira katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* ambayo haijachunguzwa sana.

## Marejeleo


Arege,T. (2013) *Tunu ya Ushairi*. Nairobi: Oxford University Press.

Erikson, H.E (1961) *Youth change and challenge*. New York: America Academy of Art and Science.

Gorky, M (1921) *Through Russia*. London: CJ Hoogarth.

Hussein, E. N (1971) *Wakati ukuta*. Nairobi: East Africa Publishing house.

Kaui T.M (2008)'Usawiri wa vijana katika tamthilia za Kiswahili'Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Keniston, K ( 1975) *Youth as a stage of life*: USA, The National Society for the Study of Education.

Kezilahabi, E (1971) *Rosa Mistika.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

___________ (1974) *Kichwamaji*. Nairobi: East Africa Publishing House.

Kiongera, K.J (2012) 'Mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya, katika tamthilia nne za Kiswahili'. Tasnifu ya uzamili,Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Kitsao, J (1980) *Uasi*. Nairobi: Oxford University Press.

Lugano, R.S (1989) 'Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi'. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Lukacs (1962) *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Press.

Mayieka, N.M(2014). 'Masuala ibuka katika *Kidagaa Kimemwozea*.' Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Marx, K. (1959) *Marx and Engels on Literature*. New York: International General.

Mazrui, A. (1984) 'Uhakiki wa *Dunia Mti Mkavu*.' Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard books, Graphics and publishers.

Mohamed, S.A (2000) *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Oxford University Press.

(2014) *Mkamandume*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Msokile, M (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Education Publishers.

Muriithi, (2016) 'Changamoto ambazo huwakumba vijana katika riwaya za *Upotevu* na *Dunia Uwanja wa Fujo.'* Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Mutua, J.M (2007) 'Mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa wanawake katika tamthilia tatu za Kiswahili'Tasnifu ya uzamili,Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Naliaka, R (2012)`Hali ya vijana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara*'Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Njogu, K (1997) Uhakiki wa riwaya za *Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Njogu, K na Chimerah, R (1999) *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkonge, G, (2006). 'Athari za Udhanaishi katika *Kichwa Maji* na *Nguvu ya Sala*.'Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Nyamemba, (2012) 'Uchanganuzi linganishi wa jinsi waandishi katika *Tunu ya Ushairi* wanavyoshughulikia masuala ya vijana.'Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Obore, E. M (2012)'Dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika Riwaya ya *Rosa Mistika'*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Osango (2015) 'Ukombozi wa kisiasa na kiuchumi katika *Mkamandume*.'Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Rono, P (2013) 'Uhakiki wa kimaudhui na kifani wa *Kidagaa Kimemwozea'*,Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Senkoro, F.E.M.K(1987) *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Center.

Wa Mberia, K. (1997) *Natala*. Nairobi: Marimba publications.

___________ (2001) *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba publications.

___________ (1999) *Maua kwenye jua la asubuhi*. Nairobi: Marimba publications.

Wafula, R.M(1999) 'Uhakiki wa tamthilia tatu kuhusu wahusika vijana'. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Wafula, R.M na Njogu K (2007) *Nadharia za Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K (2006) *Kufa Kuzikana*. Nairobi: Longhorn Publishers.

_________ (2012) *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publications Limited.

Wamitila, K.W (2001) *Nguvu ya Sala.* Nairobi: Longhorn Publishers.

_________ (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

_________ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*: Focus publishers. .

_________ (2003) *Pango*. Nairobi: Focus publishers.

_________(2008) *Misingi ya uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi.Vide- Muwa Publishers Ltd.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY